SportPesa
TZS. 686,934,380
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Hatimaye** mgogoro KKKT Dayosisi ya Konde wamalizika

UKURASA 16



**Real Madrid kutomsajili Mbappe Januari**

UKURASA 23


# Nipashe

Alhamisi Novemba 18, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580768

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




# Nafuu mgawo maji yanukia

UKURASA 2

## YALIYOMO


UKURASA WA 4
**PINGAMIZI LA UTETEZI KESI SABAYA LATUPWA**
MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, imekubali kupokea nyaraka...

UKURASA WA 4
**MWANAFUNZI WA KIKE AJERUHIWA KWA KISU**
MWANAFUNZI wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Mbogi...

UKURASA WA 9
**RC NJOMBE AHIMIZA CHANJO YA UVIKO-19**
MKUU wa Mkoa wa Njombe Marwa Rubirya, amewataka wananchi kuchukua...


## Korti yaruhusu ukaguzi ‘diary’ kesi ya Mbowe

UKURASA 3



UKURASA 2

Wafanyakazi wa Bandari ya Dar es Salaam, wakijiandaa kushusha kutoka kwenye meli moja ya vichwa vitatu vya treni ya reli ya kisasa (SGR) vyenye thamani ya Sh. bilioni 22, bandarini hapo jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Vichwa, mabehewa ya treni sasa kutengenezwa nchini

MICHEZO YANGA, NAMUNGO MTAFUTANO UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# Nafuu mgawo maji Dar, Pwani yanukia

**Na Frank Monyo**

BODI ya Maji Bonde la Wami/Ruvu mkoani Pwani imesema inafikiria namna ya kutumia maji ya bwawa la asili la Kitela.

Bwawa hilo liko Kitongoji cha Ruvu kwa Dosa Kata ya Mtambani Wilaya ya Kibaha ili kuyachepusha kuingia Mto Ruvu kuongeza wingi wa maji, kuhakikisha yanafika kwenye mtambo wa kuzalisha maji wa Ruvu Chini ili kupunguza makali ya uhaba wa maji kwa mikoa ya Pwani na Dar es Salaam.

Aidha, bodi hiyo imesema kuanzia leo, wataalamu wa ubora wa maji na maji juu ya ardhi wataelekea kwenye bwawa hilo, ili kupima ubora na wingi wake ili kuepuka uharibifu wa ikolojia.

Hatua hiyo imefikiwa ukiwa utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alilotoa Jumatatu kwa kulipa siku tatu bonde hilo kuhakikisha linafatilia njia zote za kuingiza maji katika Mto Ruvu ambazo zimechepushwa na kuruhusu maji kufuata njia yake.

Akizungumza jana wakati wa ukaguzi huo, Ofisa Maji Msaidizi wa bonde hilo Dar es Salaam, Halima Faraji, alisema bwawa la Kitela limeonekana ni msaada mkubwa kwa wananchi wa eneo hilo kwa kufanya shughuli za kilimo na kunyweshea mifugo, hivyo amewataka kupunguza matumizi ya bwawa hilo kuhakikisha maji yanaongezeka Mto Ruvu.

"Hatutaki kuathiri mfumo wa asili wa bwawa hili, tutajaribu kuangalia na kupima ili kujua kuna kiwango gani cha maji na ubora kwa kushirikiana na halmashauri na wataalamu wetu na timu imeanza safari kuelekea kwenye bwawa hilo ili kuongeza maji katika Mto Ruvu," alisema Halima na kuongeza:

"Lakini tuombe wenyeviti wa vitongoji kuanza kuratibu masuala ya mifugo kuhakikisha ng'ombe hawaingii kwenye mito ili kupunguza athari katika vyanzo vya maji."

Alisema kutokana na mabadiliko ya tabianchi yaliyosababisha maji kapungua katika Mto Ruvu, pia imechangiwa na shughuli za kibinadamu zinazofanyika, hivyo bodi hiyo imekuwa na utaratibu wa kutoa elimu ya utunzaji wa vyanzo vya maji na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika vyanzo hivyo lengo ni kuhakikisha maji yanawafikia watumiaji.

"Kilichojitokeza sasa hivi mvua zimekuwa chache kwa mwaka huu, kumekuwa na upungufu mkubwa wa maji ambao umeathiri mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro pamoja na Pwani, kwa kiwango kidogo cha maji ambacho kipo kwenye Mto Ruvu, tumehakikisha wananchi wanatumia maji kwa ufanisi kwa kupunguza matumizi," aliongeza.

Aliongeza kuwa wapo katika mpango wa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhakikisha wafugaji wanajengewa mabirika ya kunyweshea mifugo na mabwawa madogo ili wasiingize mifugo yao katika mito kwa ajili ya kunywesha maji.

Alisema kuwa bodi itahakikisha kwa kiwango hicho cha maji kidogo kilichopo kitatumika kwa ajili ya wananchi mpaka pale maji yatakapoongezeka na huduma kurudi katika hali ya kawaida.

Aidha, alisema kuwa kwa wale wenye vibali vya matumizi ya maji katika Mto Ruvu wanapaswa kuhakikisha wanapunguza matumizi ili maji yaliyopo yanaendelea kuingia katika vidakio vya Ruvu Juu na Chini ya kupunguza makali ya mgawo wa maji kwa wananchi wa Pwani na Dar es Salaam.

Ofisa Mazingira wa Wilaya ya Kibaha, Maxmillian Evarist, alisema kutokana na mabadiliko ya tabianchi yaliyosababisha maji kapungua katika Mto Ruvu, ipo haja ya wahusika kutoa elimu kwa wakulima kubadilisha aina ya kilimo cha umwagiliaji ili kutumia maji machache.



Ofisa Maji Msaidizi wa Bodi ya Bonde la Wami/Ruvu Dar es Salaam, Halima Faraji (kulia) na Ofisa Mazingira wa Wilaya ya Kibaha, Maxmillian Evarist, wakiangalia hali ya maji katika Mto Ruvu, Kijiji cha Dosa, Kata ya Mtambani, wilayani Kibaha mkoani pwani jana, kufuatia agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kutaka ukaguzi wa njia zilizochepushwa kuingia kwenye mto huo. **PICHA: FRANK MONYO**

## Mwanafunzi adaiwa kuchomwa kisu shingoni na mjomba

**Na Said Hamdani, LINDI**

MWANAFUNZI wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Liganga mkoani Lindi (jina linahifadhiwa), amelazwa katika Hospitali ya Misheni ya Nyangao kwa madai ya kushambuliwa kwa kisu na mjomba wake.

Taarifa kutoka kijijini hapo zilizothibitishwa na viongozi wa serikali, ndugu na majirani zinaeleza mwanafunzi huyo alifanyiwa kitendo hicho juzi na Hamisi Nguruwe.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mnara, Mohamed Timwanga, alisema mwanafunzi huyo alishambuliwa kwa kukatwa kisu shingoni na mjomba wake huyo, huku akisema sababu za mjomba huyo kuchukua uamuzi huo dhidi ya mtoto wa dada yake hazijafahamika.

"Huyu ni mtoto aliyezaliwa na dada yake. Nguruwe alimwomba ili akae naye kumsaidia shangazi yake baadhi ya kazi ndogondogo," alisema mtendaji huyo.

Alisema mtuhumiwa baada ya kufanya ukatili huo, aliamua kunywa sumu kwa lengo la kujiua lakini wananchi waliokuwa karibu walimnusuru uhai kwa kumnywesha chumvi iliyokorogwa kwa maji.

Timwanga alisema mtuhumiwa alikamatwa na kufikishwa katika kituo cha polisi cha Mtama na baadaye Lindi kwa hatua zaidi za kisheria.

Baadhi ya mashuhuda ambao hawakupenda majina yao yatajwe kwenye vyombo vya habari, walidai kuwa Nguruwe alikuwa anaishi na mwanafunzi huyo baada ya kumwomba dada akae naye ili kumsaidia shangazi yake kazi ndogo ndogo.

Hata hivyo, walidai kuwa mtuhumiwa alibadili utaratibu wa maisha na kuishi naye kimapenzi, jambo ambalo wazazi limewachukiza na kufanya uamuzi wa kumchukua na kuondoka naye.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna Msaidizi (ACP) Mtatiro Kitinkwi, alipoulizwa kuhusu tukio hilo, alisema bado haijamfikia ofisini kwake na kuahidi kulifuatilia.

# Vichwa treni, mabehewa sasa kutengenezwa nchini

**Na Christina Mwakangale**

TANZANIA inatarajia kuanza uzalishaji wa vichwa vya treni na mabehewa ambavyo vitauzwa katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Mwakilishi wa kampuni ya SMH Rail kutoka nchi ya Malaysia, Mussa Mansour, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof Makame Mbarawa, akipokea vichwa vitatu vya treni, aina ya H10 series.

Mansour alisema kampuni hiyo imekuwa ikifanya ukarabati wa vichwa na mabehewa ya Shirika la Reli Tanzania (TRC) tangu mwaka 2013, akisema uwekezaji unaotarajiwa kufanyika nchini una thamani ya Dola za Kimarekani milioni 40 hadi 100 sawa na Sh. bilioni 92 hadi 230 bilioni.

"Tumepanga kuwekeza hapa ili vichwa vya treni na mabehewa viwe vinatengenezwa hapa, tupo kwenye mchakato tumelenga soko la EAC na SADC. Serikali tayari imetupatia eka 50 huko Kwara, Kibaha tunaendelea na taratibu zetu na huenda tukaanza ujenzi Desemba 15, ajira zitakazozalishwa ni zaidi ya 1,000," alisema Manour.

"Endapo mipango itatimia kama ilivyopangwa ndani ya kipindi cha mwaka mmoja ujao huenda Tanzania ikiwa inafanya ambavyo vinatarajiwa kutumika kuongeza shughuli za ubebaji wa mizigo zinazofanywa na Shirika la Reli nchini (TRC).

Kampuni ya SMH ambayo makao yake makuu yapo Kuala Lumpur nchini Malaysia, inajihusisha na usanifu, uhandisi, uzalishaji na ukarabati wa vichwa vya treni na mabehewa ya Metre Guage na Standard Guage.

Awali, Prof Mbarawa alisema baada ya kupokea vichwa hivi vitatu, shirika litakuwa na jumla ya vichwa vya treni 43 vya masafa marefu na vichwa vya sogeza saba katika uendeshaji na vichwa viwili vya masafa marefu katika mwaka wa fedha 2021/2022.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2020/2021, shirika liliweza kubeba tani za mizigo 320,106 lengo lilikuwa ni tani 400,000 na lengo lililofikiwa asilimia 80. Mwaka 2021/2022 tuna uhakika wa kusafirisha tani nyingi kutokana na ujio wa vichwa hivi vitatu, vitaongeza kasi ya ubebaji mizigo kutoka katika bandari ya Dar es Salaam.

**TRC**

Mkurugenzi Mkuu TRC, Masanja Kadogosa, alisema Shirika linaendelea na uboreshaji wa huduma ya usafirishaji wa mizigo kwa njia ya reli kutoka Dar es Salaam hadi bandari mradi unaotekelezwa kwa fedha ya mkopo wa Dola milioni 300 kutoka Benki ya Dunia (WB.

Alisema serikali iliingia makubaliano na kampuni ya SMH Rail kutoka nchini Malaysia ambaye ni mtengenezaji wa vichwa kwa gharama ya Dola milioni 9.1, imefanikiwa kuleta vichwa vipya vitatu kwa njia ya meli iliyowasili Bandari ya Dar es Salaam, Jumatatu.

"Vichwa hivi vina uwezo mkubwa, kichwa kimoja kina nguvu ya Horse Power 3000 na kina uwezo wa kuvuta behewa 20 sawa na tani 1200 kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro, tofauti na awali vilikuwa vikifungwa vichwa viwili kwa sababu ya mwinuko mkali uliopo kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro," alisema Kadogosa.

"Kuanzia Morogoro kichwa kimoja kitaongezewa mzigo hadi kufikia tani 2000 ambazo ni sawa na behewa 33, mzigo huu endapo utasafirishwa kwa njia ya barabara utabebwa na malori 66 yenye uwezo wa kubeba tani 30 kila moja, kwa hiyo kwa kutumia vichwa vipya vitatu

uwezo wa TRC wa kusafirisha mizigo toka bandarini utaongezeka," aliongeza Kadogosa.

HABARI KITAIFA

## KESI YA MBOWE

# Mahakama yaruhusu 'diary' ikaguliwe kwa usiri

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi imeshindwa kumwondoa askari H4323 Koplo Msemwa, kwenye ushahidi kama mawakili wa utetezi walivyoomba, badala yake imekubali hoja moja ya mawakili hao ya kuruhusu 'diary' aliyokutwa nayo kizimbani shahidi huyo ikaguliwe na kwa usiri.

Baada ya kukaguliwa imekutwa na masuala yanayohusu shauri hilo la ugaidi, upande wa utetezi wameomba wapewe kama kielelezo na mahakama imekubali.

Uamuzi huo wa Mahakama ulitolewa jana katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na wenzake watatu mbele ya Jaji Joackim Tiganga.

Jaji Tiganga alifikia uamuzi baada ya kupitia hoja za malumbano ya kisheria, upande wa utetezi ulitaka Mahakama itamke kuwa shahidi hafai, ushahidi wake uondolewe kwenye kumbukumbu na kama Mahakama itaona kuna ugumu iruhusu diary ikaguliwe.

"Nakubaliana na upande wa utetezi kwamba upo umuhimu wa kukagua diary, kinachoonekana kilichotokea kinaonyesha kutoaminika kwa shahidi na ushahidi wake, Mahakama hii sasa inashindwa kumwondoa.

"Nawakabidhi diary hii iliyokuwa chini ya mikono ya Mahakama, wakili hataruhusiwa kupiga picha sehemu yoyote, zoezi la ukaguzi lifanyike kwa usiri, wakili mmoja mmoja, ndiyo maana kauli yangu kwamba haki isitendwe tu bali ionekane ikitendwa," alisema Jaji Tiganga.

Akisoma uamuzi huo alisema, sababu jambo lenyewe lilitokea wakati shauri likiendelea basi upande wa utetezi wapo sahihi kwamba sheria inaipa mamlaka mahakama.

Alisema jambo la pili kwa kutumia kifungu cha 127 upande wa utetezi walisema mahakama itamke shahidi hafai na ushahidi wake ufutwe.

"Mahakama kwa upande wake ikaona iangalie vifungu hivyo kama wezeshi au sio wezeshi.

"Kifungu namba 127 kinasema Mahakama Kuu katika kutekeleza majukumu yake huweka utaratibu juu ya kuendesha majukumu yake ya jinai.

"Hoja iliyopo kama shahidi vitu alivyokutwa navyo vinaruhusiwa mahakamani, upande wa utetezi wametaja vifungu sahihi bila kujali wapo sahihi ndani yake kuhusu shahidi huyu," alisema Jaji Tiganga.

Alisema anakubaliana na upande wa mashtaka kwamba shahidi anaruhusiwa kuingia na kidaftari kwenye kizimba cha Mahakama na kwamba hakuna sheria ya moja kwa moja inayokataza shahidi kuingia nayo.

"Upande wa utetezi wanasema sio utaratibu na upande wa mashtaka wanasema sahihi, pande zote mbili zinakubaliana kwamba shahidi alikuwa na kidaftari kwenye kizimba, hata alipoelekezwa alitoa mwenyewe," alisema.

Alisema jambo lililobakia je, ni kinyume cha sheria shahidi kuingia na kidaftari kwenye kizimba.

Jaji Tiganga alisema shahidi hakatazwi kuingia na kitu chochote kwenye kizimba na kwamba kabla hajafanya marejeo ataiomba ruhusa ya Mahakama, lakini katika shauri hilo hakuna kilichoonekana kama shahidi alikuwa anafanya marejeo.

"Mtakumbuka mshtakiwa anaruhusiwa kuingia na vielelezo kwenye kizimba kwa hiyo shahidi anaweza kuingia navyo mpaka muda atakapoomba kutumia, hili linaungwa mkono na sheria ya ushahidi katika kifungu namba 168(1) (2) cha Sheria ya Ushahidi.

"Nakubaliana na hoja za Wakili Peter Kibatala na Jeremiah Mtobesya kwamba hayo yalifanyika wakati shahidi ana kiapo chake, sheria inasema wakati amefungua diary alikuwa anafanya nini, Mahakama inaona kwa yeye kufungua na kuandika haikuwa sahihi.

"Kwa jambo hilo mahakama ina maamuzi kwamba nyaraka yoyote inayojitokeza kwenye mwenendo wa kesi mahakamani basi itakuwa ni nyaraka ama kielelezo cha Mahakama.

"Kwa kuwa diary hiyo ilikuwa kwenye kizimba cha Mahakama na nakubaliana na upande wa utetezi kwamba upo umuhimu wa kukagua," alisema Jaji Tiganga na kuamuru ikaguliwe.

Mawakili pamoja na ofisa mmoja wa Mahakama walikagua diary hiyo na kisha kurejea mahakamani na Jaji Tiganga aliwataka mawakili wote waende ofisini kwake wakamweleze walichokikuta kwenye diary.

Baada ya kurejea kwa mara nyingine, Wakili Mtobesya alidai wakati mahakama imewapa nafasi ya kwenda kukagua diary walikutana na masuala yanayohusu shauri hilo, kwa sababu hiyo kupitia kifungu 176(1) cha Sheria ya Ushahidi sura ya sita iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019 waliomba wapatiwe kama kielelezo.

Upande wa Jamhuri hawakuwa na pingamizi na mahakama ilipokea sehemu inayohusiana na shauri hilo kwenye diary kuwa kielelezo cha upande wa utetezi.

Shahidi wa pili katika kesi ndogo, Koplo Msemwa, aliruhusiwa kuendelea na ushahidi na kudai Novemba 12, mwaka huu, alipokea barua kutoka kwa Naibu Msajili na kitabu cha kumbukumbu za watuhumiwa Kituo Kikuu cha Polisi Dar es Salaam.

Alidai akiona kitabu hicho anakikumbuka kwa sababu mbalimbali ikiwamo mwandiko wake, Agosti 7, mwaka 2020 alipokea watuhumiwa wawili, Adamu Kasekwa na Mohammed Ling'wenya na aliwaweka mahabusu.

Moja ya pingamizi lililosababisha kuwapo kwa kesi ndogo, upande wa utetezi wanapinga maelezo ya onyo yasipokelewe kama kielelezo wakidai kwamba Ling'wenya hakuwahi kufikishwa kituoni hapo na kuchukuliwa hayo maelezo.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Kasekwa, Ling'wenya na Halfani Bwire ambao wanakabiliwa na mashtaka sita ya kula njama, kufanya vitendo vya kigaidi kati ya Mei mosi na Agosti 5, 2020.



# Pingamizi utetezi kesi ya Ole Sabaya latupwa

**Na Allan Isack, ARUSHA**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, imekubali kupokea nyaraka tano za upande wa Jamhuri kama vielelezo vya ushahidi katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya na wenzake sita.

Nyaraka zilizopokelewa ni barua kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kwenda kwa Meneja wa benki, kuomba kupewa video zilizorekodiwa kwenye CCTV Kamera, barua ya kuomba kupewa mandate file ya Francis Mroso na fomu iliyotumika kutolea fedha Sh.milioni 90, benki statement.

Kadhalika mahakama hiyo, ilikataa kupokea nyaraka moja ambayo ni kopi ya kitambulisho ambacho kiliambatanishwa katika fomu ya mandate ya Mroso.

Novemba 16, mwaka huu, mawakili wa utetezi, akiongozwa na Moses Mahuna, alipinga kupokelewa kwa nyaraka za benki, ikiwamo ya banki statement, Withdraw slip na barua kutoka TAKUKURU, akidai utaratibu wa kisheria haukufuatwa.

Pingamizi hilo, liliwasilishwa mbele ya hakimu wa mahakamani hiyo, Patricia Kisinda, wakati shahidi wa tisa wa Jamhuri katika kesi hiyo, ambaye ni Meneja wa Benki ya CRDB Tawi la kwa Murombo jijini Arusha, Marry Mayoka (40), akitoa ushahidi.

Hakimu Kisinda alisema mahakama imekubali kupokea vielelezo ambavyo vimetolewa mahakamani kama ushahidi.

Hakimu alisema vielelezo hivyo vimekidhi vigezo kutokana na kifungu namba 78 na 79 cha sheria ya ushahidi huku, ikikataa kupokea kielelezo kimoja.

Novemba 16, mwaka huu, akiwasilisha pingamizi hilo, Wakili wa Utetezi, Mosses Mahuna, alipinga kupokelewa kwa vielelezo hivyo akidai uwasilishaji wake haukufuata utaratibu wa kisheria.

Naye Wakili wa Serikali Mwandamizi, Tersila Gervas, aliieleza mahakama kwamba vielelezo hivyo viliwasilishwa kwa mujibu wa sheria ya ushahidi.

Awali akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Tersila Gervas, shahidi huyo, alidai akiwa kama kiongozi mkuu wa benki hiyo katika eneo hilo, aliidhinisha mfanyabiashara Francis Mroso, kutoa fedha taslimu Sh. milioni 90 kwa mkupuo mmoja.

Aidha, alidai baada ya kumhoji mfanyabiashara huyo kwa nini anatoa fedha hizo nyingi kwa wakati mmoja alimweleza kwamba kuna mtu anataka kumlipa na alikuwa ameambatana naye.

Mbali na Sabaya washtakiwa wengine, katika shauri hilo ni Silvester Nyengu(26), Enock Togolani(41), Watson Mwahomange(27), John Odemba, Jackson Macha(29) na Nathan Msuya(31).

Alidai kwamba kwa mujibu wa video za CCTV Kamera ilionyesha nje ya benki alikuwa Mrosso ameambatana na kijana mmoja ambaye aliingia ndani na kuchukua karatasi ya kuweka na kutoa fedha lakini hakuijaza na hakuhumiwa.

Shahidi huyo, aliieleza kwamba benki imeweka utaratibu wa kulinda fedha za wateja wao, zikiwa benki kwa kuwa wana mifumo bora na imara ya ulinzi ukiwamo wa CCTV Kamera.

Kadhalika, alidai akiwa kama meneja wa benki amekuwa akisimamia kuhifadhiwa kwa nyaraka mbalimbali za kibenki kutokana na huduma za wateja walizopatiwa katika benki hiyo.

Mbali na nyaraka hizo, alidai kwamba amekuwa akisimamia kuhifadhiwa kwa matukio yaliyorekodiwa kwenye mfumo wa CCTV kamera kwa kipindi cha miezi sita hadi mwaka mmoja.




Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zubeir, akionyesha hati yenye maazimio ya kudumisha upendo, kuvumiliana na kusameheana, iliyotolewa katika mkutano uliofanyika Makha nchini Saudi Arabia mwaka 2019, ukihusisha Mufti na wanazuoni wa dini ya kiislam kutoka mataifa mbalimbali, wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kusameheana na Kuvumiliana, mkoani Dar es Salaam, juzi. Kushoto ni Sheikh wa mkoa huo, Alhad Mussa Salum na Mwakilishi wa Taasisi ya World Muslim League hapa nchini, Sheikh Hassan Katungunya. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mwanafunzi ajeruhiwa kwa kisu

**Na Ambrose Wantaigwa,** TARIME

MWANAFUNZI wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Mbogi, wilayani Tarime (jina limehifadhiwa), amejeruhiwa vibaya kwa kisu na kijana ambaye hajafahamika na kumsababishia majeraha makubwa kwa kile kilichodaiwa ni kulazimisha uhusiano na binti huyo.

Mwanafunzi huyo kwa sasa anaendelea na matibabu na tukio hilo lilitokea katika eneo la Kebeyo wakati mwanafunzi huyo akitoka mtoni kuteka maji.

Aidha, mashuhuda wa tukio hilo walisema mwanafunzi huyo alipiga kelele za kuomba msaada, lakini hadi wanafika, alishajeruhiwa na mhusika kukimbia kusikojulikana.

Mkurugenzi wa Kituo cha Afya anakopatiwa matibabu, Dk. Stephen Mtimba, alisema msichana huyo alijeruhiwa sehemu mbalimbali za mwili kwa kitu chenye ncha kali na kwamba anaendelea na matibabu huku afya yake ikiimarika.

Kwa mujibu wa mashuhuda hao, msichana huyo alivamiwa wakati wa jioni akitoka mtoni na kijana mmoja ambaye bado jina lake halijafahamika kwa madai ya kulazimisha mahusiano ya ndoa.

Binamu wa mwanafunzi huyo, Rhobi Kegamba, alisema ndugu yake huyo alikuwa akilalamika kwa ndugu zake mara kadhaa kuhusu kunyanyaswa kijinsia na kijana huyo kiasi cha kusababisha taarifa hizo kuripotiwa katika uongozi wa kijiji wiki mbili zilizopita.

"Wakati familia ikisubiri hatua zaidi kutoka viongozi wa kijiji ndipo ghafla tukapata taarifa za kujeruhiwa kwa kisu binamu yangu mgongoni, tumboni na shingoni wakati akitoka mtoni kuchota maji," alisema Rhobi.

Jitihada za kumpata Kamanda wa Polisi Tarime/Rorya, William Mkonda, kuzungumzia tukio hilo zinaendelea.

## Mtuhumiwa ujambazi auawa kwa risasi Dar

**Na Romana Mallya**

MTU anayedaiwa kuwa jambazi aliyefahamika kwa jina la John Mpinga (34), ameuawa katika majibizano kati ya polisi na watu wanaodaiwa kuwa majambazi yaliyotokea Kinyerezi jijini Dar es Salaam.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alisema jana kuwa majibizano hayo yalitokea baada ya askari polisi kumkamata mmoja wa watuhumiwa wenzake kubaini wanafuatiliwa.

Kamanda Muliro alisema tukio hilo lilitokea juzi usiku maeneo ya Kinyerezi Mwisho Wilaya ya Ilala.

Alisema polisi walimkamata mmoja wa watuhumiwa hao na kuwaongoza wenzake waliko na baada ya wenzake wanne kubaini wanafuatiliwa, waliwarushia risasi polisi nao wakajihami kwa kuwarushia risasi," alisema.

Alisema wakati wa tukio hilo likiendelea, Mpinga, maarufu kama Mmasai, ambaye alikuwa anaongoza polisi kwenda kwenye kundi hilo, alijaribu kutoroka chini ya ulinzi ndipo alipojeruhiwa kwa risasi eneo la mguuni na kufariki dunia katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

"Uchunguzi wa awali umeonyesha mtuhumiwa huyu (marehemu) aliwahi kukamatwa na silaha mwaka 2014/15 lakini aliwahi kufanya matukio ya unyang'anyi maeneo ya Chanika, Kitunda, Kalakata na Temeke," alisema.

Muliro alisema katika eneo la tukio imepatikana bastola aina ya Browning, maganda manne ya risasi za bunduki aina ya AK47 na matatu ya bastola.

Alisema watuhumiwa wengine walifanikiwa kukimbia na msako dhidi yao unaendelea kufanyika.

Katika tukio lingine, Kamanda Muliro alisema mwananchi mmoja amesalimisha silaha aina ya Browning kwenye ofisi ya Mtendaji wa Mburahati ikiwa ni kutii agizo la serikali lililotaka wananchi kufanya hivyo ndani ya mwezi huu.

Kamanda Muliro aliwasisitizia wananchi kuwa msamaha huo hautakuwa na mahojiano ya kina wakati wa kusalimisha silaha hizo.

## HABARI KITAIFA

# Majadiliano ufufuaji mradi Bandari Bagamoyo mbioni

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema imedhamiria kufufua majadiliano kuhusu uendelezaji wa mradi wa Bandari ya Bagamoyo, ambao imesema haupukiki na kwamba mkataba wa ubia utakaosainiwa utaweka mbele maslahi ya taifa.

Kadhalika, mradi huo ni muhimu ili kukuza uchumi na kuongeza wigo wa utoaji huduma bandarini baada ya kubaini kwamba, bandari kuu ya Dar es Salaam, imezidiwa. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Geofrey Mwambe, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu miradi ya eneo hilo kwa ajili ya uendelezaji kiuchumi lenye hekta 9,800 litakalokuwa na miradi ya kisasa pamoja na makazi bora. Mwambe alisema mradi huo unatekelezwa na nchi tatu kwa ubia, Tanzania, Oman (Oman Investment Authority) na China kupitia kampuni ya China Merchant Port Holding Co. Ltd.

Alisema eneo hilo litakuwa na Maalum la Uendelezaji wa Teknolojia (ICT Park), taasisi za utafiti wa masuala ya viwanda na biashara, fedha, elimu, usafirishaji na utunzaji wa bidhaa, huduma za jamii na utalii.

"Lengo ni kubadili eneo hilo kuwa jiji la kisasa la viwanda kwa kuendeleza miradi ya kimkakati itakayofungamanisha viwanda, bandari ya kisasa na maendeleo ya makazi kwa mfumo unaopendekezwa wa Port-Zone-City.

"Awali, hakukuwa na mkataba wowote ambao ulionyesha kipindi cha kutekeleza mradi huu, zilikuwapo minutes tu za vikao. Sasa serikali tupo tayari kwa majadiliano na wenzetu wa nchi mbili, Oman na China. Alibainisha kwamba kutokana na mradi huo, Chuo cha Uvuvi, Mbegani kitahamishiwa Kilwa mkoani Lindi, kupisha mradi huo wa pamoja ambao utaundiwa bodi ya wakurugenzi kuongeza usimamizi thabiti.

"Timu ya pamoja ya majadiliano ziliundwa ili kuwezesha majadiliano kuhusu utaalamu, fedha, uchumi, biashara na sheria za uendelezaji wa mradi. Mkataba huu uliweka msingi wa majadiliano katika nyanja tatu za bandari, eneo la viwanda na miundombinu wezeshi.

"Majadiliano yanayoendelea yanahusu eneo dogo la mradi wa BSEZ kwa kuendeleza eneo la hekta 3,000 kati ya hekta 9,800 katika ya hizo viwanda 2,200 unajumuisha ujenzi wa miundombinu wezeshi ikiwamo barabara, reli, umeme, maji, gesi na mifumo ya mawasiliano, kuunganisha eneo la mradi.

"Inakadiriwa kwamba thamani ya uwekezaji katika eneo la bandari na Logistic Park utafikia kiasi cha Dola milioni 3,100. Uwapo wa bandari hii ulikuwa haupukiki kwa kuwa hivi sasa Bandari ya Dar es Salaam imezidiwa pamoja na maboresho kuanzia gati namba moja hadi saba, zimejaa. DRC (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo) inasafirisha zaidi mzigo kupitia bandari yetu kwa asilimia 34 na tunatarajia kufikisha 80 ya mizigo hiyo," alisema.

# Marufuku usafirishaji mazao ghafi misitu nje

**Na Lusungu Helela**

SERIKALI imepiga marufuku kusafirisha malighafi za mazao ya misitu kwenda nje ya nchi.

Akitangaza marufuku hiyo juzi, Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, alisema badala ya mazao hayo kusafirishwa yakiwa ghafi, yachakatwe katika viwanda na kuuza mazao yaliyotengenezwa vitu kutokana na bidhaa hizo.

Sambamba na hayo, alionya kuwa kutokana na marufuku hiyo, yeyote atakayebainika kusafirisha mazao hayo, atafutiwa leseni.

Waziri Ndumbaro alitoa marufuku hiyo kweye kongamano la Uwekezaji wa Sekta ya Misitu mkoani Iringa ambalo lililifanyika kwa siku tatu mjini Mafinga na kuwakutanisha wabobezi wa masuala ya misitu wa ndani na nje ya nchi.

Aliyataja mazao hayo kuwa ni magogo ya miti, gundi inayogemwa kwenye miti aina ya misindano na ''timber veneer''

Dk. Ndumbaro aliwataka wenye viwanda kuchakata mazao hayo kwa kuyaongezea thamani hadi hatua za mwisho nchini ili kuwanufaisha Watanzania kwa kupata ajira kwenye viwanda.

Akizungumzia marufuku hiyo, Dk. Ndumbaro amesema maono ya serikali kwa sasa ni kuendeleza viwanda, hivyo haiwezekani mazao ya misitu yakaendelea kusafirishwa kwenda nje ya nchi huku Watanzania wakibaki watazamaji tu

"Tanzania ya viwanda haitafanikiwa kama mimi Waziri mwenye dhamana nitaruhusu malighafi za mazao ya misitu kuendelea kusafirishwa kwenda nchi za nje sasa viwanda vyetu vitakua vipi," alisema.

Pia Dk. Ndumbaro amepiga marufuku biashara ya gundi inayogemwa kwenye miti aina ya misindano hadi pale uamuzi mwingine utakapotolewa.

Aliipa siku 30 Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) kuwasilisha ripoti juu ya faida na athari za ugemaji gundi hiyo.

Akitoa msimamo huo, Dk. Ndumbaro amewataka wenye uhitaji wa gundi hiyo wafungue viwanda nchini na si kusafirisha malighafi hiyo.


Accurate RECOVERY & AUCTIONS LTD.
*For Quality & reliable services*

## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA MICROFINANCE BANK LIMITED** tunatoa Notisi ya siku Ishirini na moja (21) kuanzia siku ya tangazo hili kuchapishwa gazetini kwa wadaiwa wake walio kiuka mikataba ya mikopo yao kama walivyo orodheshwa hapo chini kulipa mikopo yao ndani ya muda husika. Hivyo basi ifamike kwamba baada ya notisi hii kuisha muda wake kwa wale ambao hawataweza kulipa mikopo yao tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara mali zao zilizowekwa kama dhamana ya mikopo. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo kama zinavyo onekana kwenye jedwari hapo chini:-

| Na. | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | TAREHE YA MNADA | SAA YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Patricia Anuruphus Mpanju | Nyumba yenye Hati ya Mauziano yenye jina la Anuruphus Mpanju (Mdhamini) iliyopo eneo la Mivumoni, Wazo Wilaya ya Kinondoni, **DAR ES SALAAM.** | 08/12/2021 | Saa 3:00 Asubuhi na kuendelea |
| 2. | Veronica Adonice Mwanjela | Nyumba iliyopo Kiwanja Na. 219, Kitalu '22' yenye CT Na. 70806, LO Na. 233276, iliyopo eneo la Bunju 'B', Wilaya ya Kinondoni, **DAR ES SALAAM.** | 08/12/2021 | Saa 6:00 Mchana na kuendelea |
| | | Nyumba iliyopo Kiwanja Na. 132, Kitalu '8' yenye CT Na. 70250, LO Na. 233276, yenye jina la Wenceslaus K.M. Bihemo (Mdhamini) iliyopo eneo la Bunju 'B', Wilaya ya Kinondoni, **DAR ES SALAAM.** | 08/12/2021 | Saa 8:00 Mchana na kuendelea |
| 3. | Mohamed Abdallah Mwinyikondo | Nyumba yenye Leseni ya Makazi Na. KND008502, Ardhi Na. KND/KIN/KSH5/86 yenye jina la Zaina Ally Msolima (Mdhamini) iliyopo eneo la Kinondoni Shamba, Wilaya ya Kinondoni, **DAR ES SALAAM** | 10/12/2021 | Saa 3:00 Asubuhi na kuendelea |
| 4. | Athumani Hassan Mahimbo | Nyumba yenye Leseni ya Makazi Na. KND013438, Ardhi Na. KND/KWE/KMZ39/163 iliyopo eneo la Kawe Mzimuni, Wilaya ya Kinondoni, **DAR ES SALAAM** | 10/12/2021 | Saa 6:00 Mchana na kuendelea |
| 5. | Akida Ramadhani Mwaimu | Nyumba yenye Leseni ya Makazi Na. KND024459, Ardhi Na. KND/KWE/MGJ15/98 iliyopo eneo la Makongo Juu, Wilaya ya Kinondoni, **DAR ES SALAAM** | 10/12/2021 | Saa 8:00 Mchana na kuendelea |
| 6. | Albert J. Bisetsa | Nyumba yenye Leseni ya Makazi Na. KND029383, Ardhi Na. KND/MNY/KKP1/54 yenye jina la Augusta Joseph Bisetsa (Mdhamini) iliyopo eneo la Mwananyamala Kwakopa, Wilaya ya Kinondoni, **DAR ES SALAAM** | 11/12/2021 | Saa 3:00 Mchana na kuendelea |
| 7. | Iddi Athumani Fundi | Nyumba yenye Leseni ya Makazi Na. KND029365 Ardhi Na. KND/MZS/KMN8/12 iliyopo eneo la Kilimani Manzese, Wilaya ya Kinondoni, **DAR ES SALAAM.** | 11/12/2021 | Saa 5:00 Asubuhi na kuendelea |
| | | Nyumba yenye Hati ya Mauziano iliyopo eneo la Kimara 'B', Wilaya ya Ubungo**, DAR ES SALAAM.** | 11/12/2021 | Saa 7:00 Mchana na kuendelea |
| 8. | Mapendo E. George | Nyumba yenye Hati ya Mauziano iliyopo eneo la Mtaa wa Michungwani, Kata ya Saranga. Wilaya ya Ubungo**, DAR ES SALAAM.** | 15/12/2021 | Saa 3:00 Asubuhi na kuendelea |
| 9. | Almas Said Rufili | Nyumba yenye Leseni ya Makazi Na. ILA026562, Ardhi Na. ILA/TBT/MBZ4/17A iliyopo eneo la Tabata Msimbazi, Wilaya ya Ilala, **DAR ES SALAAM** | 16/12/2021 | Saa 3:00 Asubuhi na kuendelea |
| 10. | Mary B. Mbigili | Nyumba yenye Hati ya Mauziano iliyopo eneo la Bonyokwa - Kinyerezi, Wilaya ya Ilala, **DAR ES SALAAM** | 16/12/2021 | Saa 6:00 Mchana na kuendelea |
| 11. | Eveline E. Mgase | Nyumba yenye Hati ya Mauziano yenye jina la Elvis K. Mghase (Mdhamini) iliyopo eneo la Mongolandege - Ukonga, Wilaya ya Ilala**, DAR ES SALAAM.** | 16/12/2021 | Saa 8:00 Mchana na kuendelea |
| 12. | Wilfred Michael Batakanwa | Nyumba iliyopo Kiwanja Na. 919, Kitalu 'B' yenye CT Na. 155493, LO Na. 483898, yenye jina la Yusta Michael Batakanwa (Mdhamini) iliyopo eneo la Kizinga, Wilaya ya Ilala, **DAR ES SALAAM.** | 17/12/2021 | Saa 3:00 Asubuhi na kuendelea |
| 13. | Kadewela Salumu Omari | Nyumba yenye Leseni ya Makazi Na. ILA020068, Ardhi Na. ILA/UKG/MDF18/24 iliyopo eneo la Ukonga Mwembe Madafu, Wilaya ya Ilala, **DAR ES SALAAM** | 17/12/2021 | Saa 6:00 Mchana na kuendelea |
| 14. | Hidaya Mohamed Said | Nyumba yenye Leseni ya Makazi Na. TMK044093, Ardhi Na. TMK/MKW/BUZ27/149 yenye jina la Abrahamani Hamisi Muya (Mdhamini) iliyopo eneo la Makangarawe Buza, Wilaya ya Temeke, **DAR ES SALAAM** | 18/12/2021 | Saa 3:00 Asubuhi na kuendelea |
| 15. | Dua Said Sandari | Nyumba yenye Leseni ya Makazi Na. TMK040236, Ardhi Na. TMK/CHB/MNZ10/253 iliyopo eneo la Charambe Mianzini, Wilaya ya Temeke, **DAR ES SALAAM** | 18/12/2021 | Saa 5:00 Asubuhi na kuendelea |
| | | Nyumba yenye Hati ya Mauziano iliyopo eneo la Mponda Mianzini, Wilaya ya Temeke**, DAR ES SALAAM.** | 18/12/2021 | Saa 6:00 Mchana na kuendelea |
| 16. | Simon Yasinto Milanzi | Nyumba yenye Leseni ya Makazi Na. TMK002779, Ardhi Na. TMK/MBGK/MTT8/39A iliyopo eneo la Mwanamtoti, Mbagala Kuu, Wilaya ya Temeke, **DAR ES SALAAM** | 22/12/2021 | Saa 3:00 Asubuhi na kuendelea |
| 17. | Isihaka Abdallah Shamasi | Nyumba yenye Leseni ya Makazi Na. TMK040413, Ardhi Na. TMK/MBGK/MGN15/151 iliyopo eneo la Mgeninani, Mbagala Kuu, Wilaya ya Temeke, **DAR ES SALAAM** | 22/12/2021 | Saa 6:00 Mchana na kuendelea |
| 18. | Veronica Adonice Mwanjela | Nyumba iliyopo Kiwanja Na. 804, Kitalu 'D' yenye CT Na., LO Na. 973700, KGMC/LD/TND/D/804 yenye jina la Rose Wenceslaus Bihemo (Mdhamini) iliyopo eneo la Tundwi Songani, Wilaya ya Kigamboni, **DAR ES SALAAM.** | 23/12/2021 | Saa 4:00 Asubuhi na kuendelea |
| 19. | Hamisi Ally Said | Nyumba/Shamba Hati ya Mauziano iliyopo eneo la Mtaa wa Kijaka - Kimbiji, Wilaya ya Kigamboni**, DAR ES SALAAM.** | 23/12/2021 | Saa 8:00 Mchana na kuendelea |
| 20. | Peter Samwel Mwaitwalile | Nyumba yenye Hati ya Mauziano ya tarehe 26 Juni, 2005 iliyopo eneo la Kilungule - Mwandege, Vikindu, Wilaya ya Mkuranga, **PWANI** | 24/12/2021 | Saa 4:00 Asubuhi na kuendelea |

**MASHARTI YA MNADA: -**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo (as is where is basis)
2. Mteja anatakiwa kulipia asilimia 25% siku ya mnada na asilimia 75% iliyobaki amalizie ndani ya siku 14.
3. Endapo mteja atashindwa kumalizia asilimia 75% ya kiasi kilichosalia ndani ya siku 14, hatarudishiwa kiasi cha fedha alicholipa mwanzo na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama zote za kubadili HATI MILIKI ni JUU YA MNUNUZI
5. Kijana yeyote aliye chini ya miaka 18 hatoruhusiwa kushiriki mnada.
6. Kwa yeyote atakaye haribu mnada hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:-**

Mkurugenzi Mtendaji
ACCURATE RECOVERY & AUCTIONS LIMITED
S.L.P. 22226
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2171757, Cell: +255 754 848 084, +255 713 327 722
E-mail: recoveryaccurate@gmail.com

MWANGA HAKIKA MICROFINANCE BANK LIMITED
S.L.P 11735
DAR ES SALAAM
Simu: +255 747 666 511
E-mail: info@mhbbank.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wadau habari wasikilizwe

**WADAU** wa habari wamewasilisha mapendekezo ya mabadiliko ya sheria zinazosimamia taaluma ya habari nchini na yamepokelewa na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Tekonolojia ya Habari, Dk. Ashatu Kijaji, na sasa kinachosubiriwa ni hatua zaidi.

Tunaishukuru serikali kwa kuwa na sikio la kusikiliza na kupokea maoni ya wadau hawa, ambayo kwa nyakati tofauti tofauti yamekuwa yakiwasilishwa na taasisi zilizofanya uchambuzi wa sheria hizo na kuonyesha kwa kiasi gani kuna vifungu vinahitaji kurekebishwa ili kuondoa mkwamo kwenye tasnia hiyo muhimu katika jamii.

Baadhi ya vifungu vinavyopigiwa kelele na wadau ni makosa ya kitaalum kuwa makosa ya jinai, mamkala ya Mkurugenzi wa Idara ya Habari (Maelezo), ambaye anaweza kukifungia chombo cha habari kinapodhaniwa au kutuhumiwa kitenda kosa bila kufikishwa kwenye vyombo vya sheria hasa mhimili wa mahakama wenye mamlaka ya kikatiba katika suala la utoaji wa haki.

Pia ni kuwapo kwa vyombo vingi vinavyosimamia taaluma ya habari na wadau wanaona kuna umuhimu wa kuwa na kimoja ambacho kitasimamia ipasavyo.

KIlio cha wanahabari siyo bure, kwa kuwa kuna mahali sheria hizo zinawaumiza hasa kwenye mamlaka ya mkurugenzi na waziri, ambao wakati mwingine huumiza wafanyakazi waliopo kwenye vyombo husika, huku serikali ikikosa mapato ya kodi za mishahara na nyinginezo zitokanazo na biashara husika.

Tunashukuru waziri amesema serikali itashughulikia mapendekezo hayo kwa lengo la kuiwezesha sekta ya habari kuwa rafiki kwa wadau wake, hususan waandishi wa habari.

Kijaji alikaririwa akisema kuwa lengo la serikali ni kuhakikisha kwamba sekta ya habari inakuwa rafiki na ni dhamira ya wote kusonga mbele na kufikia malengo ya ufanisi utakaokuwa na faida kwa kila mmoja.

Tangu kupitishwa kwa sheria hizo mwaka 2015 na 2016, wadau hao wamekuwa wakifanya uchambuzi wa sheria hizo na kuwasilisha mapendekezo ya mabadiliko serikalini, na mara kadhaa yamepokelewa, lakini kwa kipindi chote hakukuwa na mabadiliko, hali iliyoendeleza malalamiko ya wadau.

Tunatarajia ushirikishwaji kamilifu kwenye mabadiliko ya sheria hizi, ili kuondoa maumivu ambayo yanakwaza uhuru wa upatikanaji wa taarifa na uhuru wa kujielezwa kwa Watanzania na wanahabari kwa ujumla.

Tunafikiri sasa maoni ya wadau hawa yatasikilizwa na kufanyiwa kazi ili kuona mabadiliko yanatokea kwenye sheria hizo, kwa kuwa lengo ni kuongeza uwajibikaji kwa pande zote na siyo kutaka uwapo wanataaluma ambao hawawajibiki.

Haitarajiwi kuona nyaraka hizo kuhifadhiwa kabatini kama nyingine zilizowahi kupokelewa, na sasa tunatarajia kuona ushiriki wa wadau wote wa habari katika mchakato uliobaki kwa tasnia ina wadau na taasisi nyingi, ambazo zimefanya kazi ya kuhakikisha inaieleza serikali kuhusu nyaraka hizo na umuhimu wa kufanya mabadiliko.

Tunataraji kuona ushirikiano wa dhati kwa serikali na viongozi wake kwa tasnia ya ya habari kupitia vyama vyao pasipo kubakisha wengine nyuma, lengo hili litasaidia kuimarisha ushirikiano kati ya wahusika.

Chombo cha habari kinapofungiwa maumivu siyo kwa wamiliki, bali mnyororo mrefu wa watu ambao wanaishi kwa kipato kinachotengenezwa na chombo husika, kwa kuwa walioajiriwa nao wana wategemezi wao huku wanaofanya biashara na chombo nao wanapata kula yao kwa uwapo wake.

Tunatambua kuwa vyombo hukosea, lakini mchakato wa kuhukumu ufuate taratibu za haki na uwazi, ndiyo maana kilio kikubwa cha wadau kimekuwa kwenye mamlaka makubwa kwa viongozi ambao hufungia vyombo vya habari.


Kama wanahabari tunawajibu wa kuilinda taaluma yetu kwa wivu mkubwa kwa kukemea matendo yoyote ya kuidhalilisha, na kuhakikisha kila mmoja anatekeleza wajibu wake kwa mujibu wa sheria na maadili badala ya kutumia kalamu kuumiza wengine au kuwabeba wengine.

Uandishi wa habari wenye kujali wengine na maslahi mapana ya nchi, ni hatua kubwa kuleta manufaa chanya kwa nchi, kwa kuwa bado jamii ina imani na vyombo vya habari pamoja na matarajio makubwa.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com


## Muungwana Lazima Nilonge

# Timu kubwa ya wadau yahitajika kuhamasisha chanjo UVIKO-19



Na Sabato Kasika

**CHANJO** ya kukabili maradhi ya UVIKO-19 iliyozinduliwa rasmi na Rais Samia Suluhu Hassan, mwishoni mwa Julai mwaka huu, inaendelea kutolewa kwa Watanzania katika maeneo mbalimbali nchini.

Ushirikishwaji wa wadau wengi zaidi unaweza kuwa na mchango mkubwa katika kampeni za kudhibiti ugonjwa huo hatari, uliokwishasababisha vifo vya watu katika nchi mbalimbali duniani.

Wadau wanaoweza kushirikishwa katika kampeni ya chanjo ya ugonjwa huo, ni viongozi wa vyama vya siasa, kutokana na kwamba wana wafuasi wengi mashirika yasiyo ya kiserikali, kampuni binafsi na viongozi wa dini.

Hao wakishiriki kikamilifu katika utoaji elimu ya chanjo ya ugonjwa huo, mchango wao katika jamii dhahiri ni mkubwa, hivyo ni vyema wakashirikishwa, ili nao wawaelimishe wafuasi wa vyama au dini zao.

Pia kuna viongozi wa serikali za vitongoji, vijiji na mitaa nao hawana budi kubuni mbinu mbalimbali za kufanikisha chanjo kwenye maeneo yao, ikiwamo kuingia nyumba kwa nyumba kutoa elimu, maana wako karibu na watu walioko katika maeneo yao.

Njia nyingine wanayoweza kuitumia ni kupita mitaani na kuhamasisha chanjo kwa kutumia vipaza sauti, ili kusaidia wananchi kupata elimu sahihi kuhusu chanjo hiyo, hata mwisho wa safari wengi katika umma wajitokeze kuchanjwa.

Kuwapo wadau wengi zaidi kuna nafasi ya kuhamasisha utoaji elimu kuhusu chanjo hiyo na kunaweza kuwasaidia Watanzania kuepuka elimu ya mitaani, ambayo inapotosha ukweli kuhusu chanjo hiyo.

Kuwapo chanjo ya UVIKO-19 ni hatua muhimu inayolenga kupambana na ugonjwa huo, ambao ni wazi kwamba kwa kiasi kikubwa umeathiri maisha ya watu katika nchi kwa kiwango cha juu.

Hivyo kwa nchi kukabiliana na ugonjwa huo, ni vyema wakati huu ambao chanjo inaendelea kutolewa, iende sambamba na utoaji elimu kufika mbali kwa kushirikisha wadau mbalimbali, wakiwamo baadhi nilivyowataja awali.

Ikumbukwe kuwa mwanzo wa mchakato wa chanjo hiyo, kulikuwapo taarifa nyingi za upotoshaji, ambazo wakati mwingine zinaweza kusababisha baadhi ya watu kusita kujitokeza kuchanjwa.

Lakini, ninaamini kwamba kulikuwapo wadau wengi katika kuhamasisha na kutoa elimu ya chanjo, upotoshaji hautakuwa na nguvu katika jamii na badala yake kasi ya watu kuchanjwa itazidi kuongezeka.

Sidhani kama huu ni wakati wa watu kusema 'hawaumwi' au 'hawajawahi kupata UVIKO-19' na kwamba hawaoni haja ya kuchanja, badala yake kila Mtanzania aone umuhimu wa kuchanjwa kwa kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya.

Vilevile, najua wapo wanaoibuka na madai kuwa chanjo zina madhara kama vile kusababisha vifo, kuvuruga hedhi, zinaharibu nguvu za uzazi kwa wanaume na wanawake na zinashambulia mfumo wa vinasaba na hivyo zinawafanya watu kuwa 'mazombi'.

Hayo yote yanaweza yakaisha, kwa watu kuhamasisha na kuelimishwa umuhimu wa chanjo, ili kujilinda na kuwalinda wengine na maambukizi, hata kuachana na dhana inayobeba orodha ya simulizi za madhara ambayo hayana uthibitisho wa ukweli kwa hao watumiaji.

Ni kweli kwamba chanjo ni hiari, lakini suala la kuhamasisha au kuelimisha umma wa Watanzania ni la muhimu, ambalo mwisho wake linamfanya kila mmoja kufanya uamuzi wa kuchanja au kutochanja.

Kwa mantiki hiyo, ushirikishwaji wa wadau wengi kutoa elimu sahihi ya chanjo unahitajika, kwani utasaidia pia kuwafanya Watanzania kujua ukweli na kuachana na dhana potofu dhidi ya chanjo inayoendelea kutolewa kitaifa.

Binafsi ninaamini kwamba kuwapo wadau wengi katika uhamasishaji huo, kunaweza kuziba mianya yote ya dhana potofu ambayo imeenezwa na baadhi ya wasiowatakiwa Watanzania mema na kukwamisha watu kupata chanjo.

Hivyo, wadau wengi zaidi wakishirikishwa, huku wakiwamo wanaoingia nyumba kwa nyumba kutoa elimu, watasaidia kuongeza ndani ya jamii wa kukwepa dhana potofu na kuchanjwa.

# Serikali kumaliza umaskini kupitia mfuko wa TASAF

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI ya awamu ya sita imesema imedhamiria kumaliza kabisa umaskini nchini kupitia mpango unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Akizungumzia dhamira hiyo ya serikali mbele ya Mtendaji Mkuu wa Benki ya Dunia aliyeongozana na viongozi wengine kwenye ziara maalumu ya kujionea shughuli zinazofanywa na TASAF, Mtaa wa Nzasa Manispaa ya Temeke, Dar es Salaam, Waziri wa Utumishi na Utawala Bora, Mohamed Mchengelwa, alisema watahakikisha hilo linasimamiwa ipasavyo.

"Taifa linakumbana na maadui watatu, ujinga, umaskini na maradhi, mpango wa TASAF umetuonyesha matokeo chanya kutokana na namna ulivyowasaidia wanufaika na ndiyo maana serikali hii ya awamu ya sita imeona inawezekana kumaliza umaskini kupitia mpango huu huu," alisema Mchengelwa.

"Unaweza kuona kwamba kiwango cha fedha wanachopewa walengwa ni kidogo, lakini zimewasaidia kwa kiwango kikubwa, wapo ambao mpaka sasa hawaitwi maskini tena na wameondoka kwa hiari baada ya kuitumia vizuri fedha hii wanayopewa, walikuwa hawana nyumba kwa sasa wamejenga na wanapata milo mitatu ya chakula."

Aliiomba Benki ya Dunia kuendelea kuunga mkono mpango huo ambao pamoja na mafanikio yote hayo pia umewezesha kaya zenye watoto kufanya vizuri katika masomo yao na wengi wao kuchaguliwa kuingia vyuo vikuu.

Mtendaji Mkuu wa Benki ya Dunia, Mari Pangestu, aliipongeza TASAF kwa kusimamia vyema mpango huo na kuiahidi Serikali ya Tanzania kwamba benki hiyo ipo tayari kuendelea kusaidia ili kuhakikisha wanafikia lengo la kumaliza umaskini nchini.

Alisema benki hiyo itasaidia zaidi katika eneo la elimu kwa walengwa matumizi sahihi ya fedha pamoja na kutumia ujasiriamali kujiongezea kipato.

Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Ladslaus Mwamanga, alisema mfuko utahakikisha unaendelea kusimamia vyema fedha za mfuko kwa kuhakikisha zinafanya kazi iliyokusudiwa.

"Tumeshuhudia namna ambavyo maisha ya kaya hizi za walengwa zilivyoboreka, kwa hiyo ili kusaidia kaya nyingi zaidi kama ambavyo serikali imeamua kuzifikia zote zenye hali duni nchi nzima, TASAF tunapambana kuhakikisha wengi wanaondoka kwenye hali hiyo na tutafanikiwa," alisema Mwamanga.


## LOSAREA COMPANY LIMITED

**Email: losareaauctionmart@gmail.com**
**Phone: 0767 98 18 89, 0694 45 84 72.**
*Dealers in debt collection, Auctioneers, Repossession, Court Brokers, Real Estate Agents and General Business*

## NOTISI YA SIKU 21 YA KULIPA DENI / TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA MICROFINANCE BANK** tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara dhamana za wadaiwa wake kama zinavyooneshwa kwenye jedwali hapo chini kama hawatalipa madeni yao ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya Notisi au tangazo hili. Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo baada ya siku 21 kuanzia tarehe ya Notisi/Tangazo hili.

| NA. | JINA LA MDAIWA. | AINA YA DHAMANA | TAREHE YA MNADA | MAHALI ILIPO DHAMANA | MUDA WA MNADA | BENKI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | JOHN JOSEPH MISIKANE. | Landed Property.Registration. R. LICENSE No.TMK044501 | 18/12/2021 | Parcel No.TMK/MKW/MAK6/200. Located at Makangarawe, Makangarawe in Temeke Municipality | Kuanzia saa nne (4:00) asubuhi na kuendelea. | MWANGA HAKIKA MICROFINANCE BANK |
| 2. | NACOD ENTERPRISE LIMITED. | Landed Property.Registration Tittle No.76920, L.O. NO. 279268 Plot NO. 165. | 16/12/2021 | PLOT NO. 165, Block 2, Mivumoni Area. Kinondoni. | Kuanzia saa nne (4:00) asubuhi na kuendelea. | MWANGA HAKIKA MICROFINANCE BANK |
| 3. | JOYCE G. LIMBUMBA | Landed Property.Registration C.T No. 70220 L.O. NO. 231216 Plot NO. 131 | 18/12/2021 | Plot No.131, Block 2, Located at Mwanagati in Ilala Municip | Kuanzia saa saba (7:00) mchana na kuendelea. | MWANGA HAKIKA MICROFINANCE BANK |
| 4. | BABU S. YUSUPH | Landed property Registration. R. LICENSE No.KNDO29625 | 16/12/2021 | Parcel No.KND/MNY/MSA 7/74B Located at Msisiri A, Mwananyamala in Kinondoni Municipality. | Kuanzia saa nane (8:00) mchana na kuendelea. | MWANGA HAKIKA MICROFINANCE BANK |
| 5. | JULIUS GIDEON MWAKALONGE | Landed property Registration R. LICENSE No. ILA008855 | 20/12/2021 | Parcel No.ILA/UKG/MZZ34/153 Located at Mazizini, Ukonga in Ilala Municipality. | Kuanzia saa nne (4:00) asubuhi na kuendelea. | MWANGA HAKIKA MICROFINANCE BANK |

**MASHARTI YA MNADA: -**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo mahali ilipo.
2. Mteja anatakiwa kulipia asilimia 25% siku ya mnada na asilimia 75% iliyobaki amalizie ndani ya siku 14.
3. Endapo mteja atashindwa kumalizia asilimia 75% ya kiasi kilicho salia ndani ya siku 14, hatarudishiwa kiasi cha fedha alicholipa mwanzo na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama zote za kubadili HATI MILIKI ni JUU YA MNUNUZI.
5. Mtoto au Mtu yeyote aliye chini ya miaka 18 hatoruhusiwa kushiriki mnada.
6. Mtu yeyote atakaye haribu mnada hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA;**

**MKURUGENZI MTENDAJI,**
**LOSAREA COMPANY LTD.**
**P. O. BOX 523, ARUSHA.**
**SIMU: 0767 981 889, 0694 486 520.**

**AU**

**MKURUGENZI MTENDAJI,**
**MWANGA HAKIKA MICROFINANCE BANK LTD.**
**S.L.P 11735, DAR ES SALAAM.**
**SIMU: +255 747 666 511.**



## CONTRACTORS REGISTRATION BOARD

## Contractors Training Course

**Dar es Salaam, 01– 03, Dec 2021**

**Module SC 140/ MC 240: Contracts Management**

***PSSSF Convention Centre (PPF Tower) - Dar es Salaam***

The Contractors Registration Board wishes to inform all Contractors that a training course on Contracts Management (Module SC 140/ MC 240) will take place in Dar es Salaam at **PSSSF Convention Centre** starting at **8:30 on Wednesday 01st to Friday 03rd December 2021**

The course is highly interactive and practice-oriented and will focus on areas that will enable contractors and other practitioners to improve their Contracts Management skills. The course will cover basic features of construction contracts, rights and obligations of parties to a contract, contract documents, contract performance, contract administration and procedures, variations, dispute resolution, sub-contracts, claims, preparation of interim and final payment certificate valuations Training on the use of **Tanzania National Electronic Procurement System** (TANEPS) will also be covered.

The course is targeted at Managing Directors (MDs) and Directors of Contracting firms registered with CRB, Architects, Engineers, Quantity Surveyors, Technicians and other Technical personnel from Institutions dealing with Construction

The fees for the course is TZS 50,000/= per participant for registered contractors and TZS 100,000/= for non contractors.

The fee covers training materials, lunch and beverages for three days. Fees are to be paid directly to CRDB, NBC and NMB Banks in the name of CONTRACTORS REGISTRATION BOARD using control numbers 995740044391 for contractors and 995740044496 for non contractors

For further inquiries, please contact:
*Contractors Registration Board, 3rd Fl., Tetex Hse, Pamba Road, P. O. Box 13374, DSM*
*Tel No: 2131169/ 2137962-3, Fax No: 2137964, E-mail: **crbhq@crbtz.org;** Web-site: **www.crb.go.tz** or*

*Contractors Registration Board, East Zone Office, Keko Mwanga-Nyerere Road, Mpingo House, 5th Floor,*
*P. O. Box 33621, DSM*
*Tel/ Fax No: +255222771877/2701747, E- mail **crbez@crbtz.org** or*


*Contractors Registration Board, Lake Zone Office, TANROADS Compound,*
*P. O. Box 2815, MWANZA*
*Tel/ Fax No: 028-2502212, Tel No: 028-2500218, E-mail: **crblz@crbtz.org** or*

*Contractors Registration Board, Southern Zone Office, NHIF Tower, 3rd Floor,*
*P. O. Box 1690, MBEYA*
*Tel No: 025-2502480, Fax No: 025-2502580, E-mail: **crbsz@crbtz.org** or*

*Contractors Registration Board, Northern Zone Office, Mafao House, 11th Floor,*
*P. O. Box 16795, ARUSHA*
*Tel/ Fax No: 027-254710 , E-mail: **crbnz@crbtz.org** or*

*Contractors Registration Board, Central Zone Office, CRB Building, Mezzanine Floor, P. O. Box 2618, DODOMA*
*Tel/ Fax No: +255262966040-1, E-mail: crbcz@crbtz.org*

**REGISTRAR**



Msajili wa Hazina, Mgonya Benedicto (kushoto), akipokea hati ya makabidhiano ya mali za shamba la ngano la Basotu lilioko wilayani Hanang kutoka kwa Wakili Joseph Tadayo wa Kampuni ya Uwakili ya Tadayo, wakati wa hafla ya makabidhiano ya mali za shamba hilo kutoka kwa Mfilisi, katika Ofisi za Msajili wa Hazina, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OFISI YA MSAJILI HAZINA**

# Halmashauri Hanang yapewa usimamizi shamba la ngano

**Na Mwandishi Maalumu**

SERIKALI imeikabidhi Halmashauri ya Wilaya ya Hanang usimamizi na uangalzi wa muda wa mali zote zilizoko katika shamba la ngano la Basotu wilayani humo lenye ukubwa wa hekta 5,138.

Halmashauri hiyo imepewa jukumu hilo wakatserikali ikiandaa mipango ya muda mrefu ya matumizi ya shamba hilo.

Hatua hiyo imechukuliwa baada ya mali katika shamba hilo kuwa chini ya uangalizi wa Mfilisi, Kampuni ya

Uwakili ya Tadayo kwa zaidi ya miaka 15.

Mwaka 2004, Mfilisi Wakili Joseph Tadayo ambaye ni Mbunge wa sasa wa Mwanga, alikabidhiwa kwa ajili ya kuuza shamba na mali zake, lakini baadaye mwaka 2007, serikali ilisitisha uamuzi huo na kuziacha mali hizo chini ya uangalizi wa Kampuni ya Uwakili ya Tadayo.

Msajili wa Hazina, Mgonya Benedicto, jana alipokea mali za shamba hilo la Basotu kutoka kwa Wakili Tadayo, makabidhiano yaliyofanyika katika Ofisi za Msajili wa Hazina, jijini Dar es Salaam.

"Ofisi yangu inashukuru kwa kazi ya uangalizi iliyofanywa na Kampuni ya Tadayo licha

ya kuwapo kwa changamoto kadhaa," alisema Msajili wa Hazina baada ya kupokea hati ya makabidhiano.

Hati hizo zinaonyesha kuwapo kwa mali mbalimbali katika shamba hilo zikijumuisha mitambo na majengo 37, nyumba za makazi 28, maghala mawili, vihenge (silos) sita, ukumbi wa starehe, mgahawa, kanisa, duka na mitambo mbalimbali pamoja na matrekta na mashine za kuvunia nafaka.


**STEAM**

**Generation Recoveries Ltd**

2nd Floor, Shamo Tower, Plot No 246/247 Block D Mbezi Beach New Bagamoyo Road, P. O. Box 80607 Dsm, Tz
Tel/ Fax: +255 222 618611/ Mob: +255 715 91 74 51, Email: steam@steamtz.com website: steamtz.com

**NOTISI /TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA MICROFINANCE BANK** Tunatoa notisi ya siku 14 kwa mdaiwa kulipa deni la Benk, baada ya hapo tutauza kwa mnada wahadhara dhamana/ mali ya mdaiwa alieshindwa kurejesha mkopo wa Bank hiyo.

Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kama ifuatavyo:

| Na | JINA LA MDAIWA | JINA LA MWENYE DHAMANA | DHAMANA | TAREHE/MUDA | BENKI. |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | HUSSEIN RASHID HUSSEIN | HUSSEIN RASHID HUSSEIN | GARI NO. T835 CKR TOYOTA IST, MBEZI BEACH. | 01/12/2021 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI | MWANGA HAKIKA BANK |

**MASHARTI YA MNADA**

i. Mali Dhamana itauzwa kama ilivyo.
ii. Mshindi atatakiwa kulipa malipo ya awali ya (25%) ya kiasi alichoshinda na salio la 75% kulipwa ndani ya siku 14 tokea siku yamnada.
iii. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti na mbili hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.
iv. mnada. Malipo yote yanayohusu nyumba/viwanja au gari ni lazima yafanyike kwenye akaunti maalum ya makusanyo itakayotolewa na Afisa wa benki.
v. Gharama zote za kubadilisha taarifa za nyaraka za umiliki au kumuondoa mkazi katika nyumba zitagharamiwa na mnunuzi.
vi. Kwa maelezo Zaidi wasiliana na Dalali kwa mawasiliano yaliyotolewa hapo juu .


## Kikwazo mimba utotoni chatajwa

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

OFISA Ustawi wa Jamii mkoani Shinyanga, Lidya Kwesigabo, amesema ukosefu wa nyumba salama ya kuhifadhi waathirika wa mimba za utotoni ni kikwazo kwa watuhumiwa kutiwa hatiani.

Alibainisha hayo jana, kwenye kikao cha dharura cha kujadili matukio ya mimba na ndoa za utotoni mkoani Shinyanga na kuweka mikakati ya pamoja na asasi za kiraia, serikali na Jeshi la Polisi kutokomeza matukio hayo.

Kwesigabo alisema kesi nyingi za mimba za utotoni mkoani Shinyanga, zimekuwa zikiishia njiani kutokana na watoto waliopewa mimba hizo, kuwakana wahusika baada ya kushawishiwa na wazazi wao baada ya kupeana kitu kidogo ikiwamo mifugo.

"Naziomba asasi za kiraia mnapokuwa mkiandika maandiko yenu ombeni pia na ufadhili wa kujenga nyumba salama ya kuhifadhi waathirika wa mimba za utotoni ili wabaki hapo hadi kesi inakwisha na kutorudi nyumbani kwao," alisema Kwesigabo.

"Kesi nyingi za mimba za utotoni zimekuwa zikiishia njiani kwasababu waathirika wa mimba hizi mara ya kwanza anamtaja fulani ndiyo kampa ujauzito, lakini akirudi tu nyumbani kwao, akija tena kwenye kesi anamkana mtu huyo na hatimaye mtuhumiwa kuachiwa huru," aliongeza.

Naye Wakili wa Serikali Ofisi ya Taifa ya Mashtaka mkoani Shinyanga, Salome Mbughuni, alisema ukosefu wa ushahidi kwenye kesi za matukio ya ukatili, umekuwa changamoto kubwa ambapo kesi ikifikisha siku 60 bila ushahidi inafutwa.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, George Kyando, alisema katika dawati la jinsia la jeshi hilo, wamekuwa wakikumbana na changamoto hiyo ya waathirika wa mimba za utotoni kukana watuhumiwa.

Alitoa ushauri kwa serikali kuifanyia marekebisho Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, ambayo ina mlinda mtoto aliyefanya kosa chini ya umri wa miaka 18, hivyo kushindwa kuchukuliwa hatua watoto hao, pale wanapowakana watuhumiwa.

# Ushuru waathiri mazao misitu

**Na Christina Haule,** MOROGORO

VIJIJI 20 vya Mradi wa Kuhifadhi Misitu kwa Kuwezesha Biashara Endelevu ya Mazao ya Misitu Tanzania (CoForEST) wilayani Kilosa, vimejipanga kupeleka biashara ya mkaa sokoni ili kukabiliana na mabadiliko ya bei mpya ya ushuru.

Tangazo la serikali (GN 417) la mwaka 2019, linawafanya wasimamizi wa mazao ya misitu kukimbilia kwenye kilimo cha miwa baada ya kukosa masoko na kuhatarisha hali ya usimamizi shirikishi wa misitu ya vijiji.

Kukosekana kwa wateja wa mazao ya misitu kumesababisha shughuli za usimamizi wa mazao ya misitu (USM) kupungua na kutishia kupoteza usimamizi wa misitu kwenye kijiji kutokana na wasimamizi wa sasa kukimbilia kwenye shughuli za kulima miraba ili kujipatia fedha za kujikimu.

Katibu wa Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA), Kulangwa Ganda, alisema hayo jana mbele ya waandishi wa habari waliotembelea msitu wa kijiji cha Ihombwe kwa ajili ya kujionea shughuli mbalimbali zinazofanywa na wananchi katika utunzaji wa msitu chini ya mtandao huo kwa kushirikiana na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi (SDC).

Ganda alisema changamoto ya GN 417 ya mabadiliko ya bei elekezi kuwa Sh. 12,000 kwa gunia la kilo 50 kutoka bei ya kijiji ya Sh. 6,750 imesababisha mapato kuanza kupungua hali inayosababishwa na kukosekana kwa wateja wa kununua mkaa na mbao endelevu.

Aliiomba serikali kuviachia vijiji utaratibu wa kujipangia bei kwa sheria ya mwaka 2002 ambayo inaviruhusu vijiji kuwa na mamlaka ya kufanya hivyo kwa kuwa GN 417 imekuwa ikiathiri ulinzi wa misitu.

Ganda alisema wamekuwa wakitumia Sh. 5,000 ambazo zinatokana na fedha za mazao ya misitu kumpa kila mmoja anayekwenda kwenye doria ili kuweka ulinzi kwenye mazao ya misitu na kuzuia ujangili jambo ambalo kama hawatakuwa na mapato, hawataweza kulifanya.

Naye Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Ihombwe, Vashty Chimilo, alisema tangu mwaka 2019, GN 417 ilipoanza kutumika, mapato yameshuka kwa kila mwezi kutoka Sh. 1,351,000 kwa mwezi na kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kijiji kilikusanya Sh. milioni tisa ambazo ni ndogo tangu kuanza kwa mradi mwaka 2014.

Alisema kuanzia mwaka 2014 mpaka 2021, Sh. 89,152,7500 zilikusanywa na zimetumika katika mambo mbalimbali ya maendeleo na kubaki Sh. milioni 70 ambazo ziko benki kwa ajili ya matumizi mengine.

Chimilo alisema kijiji hicho kina wakazi 3,100 kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, na kwamba wamekuwa wakifanya matumizi ya fedha wanazopata kutokana na msitu na kupitia fedha hizo wamechonga barabara yenye urefu wa kilometa tisa ili kufanya barabara kupitika na kupata wateja.

Alisema fedha hizo pia zimetumika katika kulipia wananchi wa kijiji wapatao 3,100 kuwalipia bima za afya (CHF) wakiwamo wazee, wenye ulemavu, wajane, watu wasiojiweza na watoto na kila mwaka wamekuwa wakilipia kaya 30.

Aidha, alisema kijiji hicho chenye ukubwa wa eneo na hekta 20,001 na kati ya hizo eneo la misitu lililotengwa ni hekta 9,597 ambazo wamegawanya maeneo madogo ya uhifadhi, uchomaji mkaa endelevu, uchanaji mbao, kutunza vyanzo vya maji na baionuai.

"Baada ya bei kubadilika wafanyabiashara wengi wameondoka baada ya kutokuwapo kwa utofauti na sasa wamekimbilia mkoani Iringa kununua mkaa wa maeneo hayo ujulikanao kama mwati ambao gunia lake ni kubwa, hivyo kufanya ushindani wa soko,"alisema.

# Majaliwa asisitiza riba benki kushuka

**Na Faustine Feliciane**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameiagiza Wizara ya Fedha na Mipango kukaa na benki na kuangalia namna ya kuweka masharti na riba nafuu ya mikopo kwa taasisi au kampuni zinazotaka kuanzisha viwanda nchini.

Akizindua jengo la kiwanda cha kutengeneza kemikali za ujenzi cha Sika kilichojengwa Mbezi-Salasala jijini Dar es Salaam, alisema inaendelea na mpango wa kutaka kuona Tanzania inakuwa ya viwanda kwa ajili ya ustawi wa uchumi na kwamba ni lazima waweke mazingira mazuri kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Alisema kuwapo kwa masharti na riba nafuu kutavutia taasisi na kampuni kukopa kwa ajili ya uwanzishwaji wa viwanda, hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi.

"Mbali na maagizo haya kwa Wizara ya Fedha, lakini pia zipo jitihada zinazofanywa na wawekezaji kwa kujenga viwanda nchini na kushiriki kwa vitendo maono ya serikali ya kutaka kuwa na viwanda vingi,"alisema.

# Wakazi Mwanza kupima afya bure

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WAKAZI wa jiji la Mwanza wametakiwa kujitokeza ili kupima magonjwa mbalimbali bure kwa siku tano yakiwamo VVU, saratani ya kizazi pamoja na kufundishwa njia za uzazi wa mpango.

Msaada huo wa matibabu ulianza kutolewa bure juzi na Shirika la Marie Stopers Tanzania, ambalo limefungua ofisi zake mpya mkoani humo.

Msimamizi wake, Dk. Emmanuel Kimario, alisema saratani ya mlango wa kizazi ni miongoni mwa magonjwa yanayosababisha vifo vya wanawake nchini

"Katika ufunguzi wa kituo hiki, tumetoa ofa kwa wananchi kuanzia Novemba 15 had 19, mwaka huu, kuja kupimwa afya zao bila ya malipo yoyote kwa magonjwa ya saratani ya mlango wa kizazi na matiti, upimaji wa VVU kwa hiyari na kupewa ushauri nasaha wa daktari," alisema Kimario.

Aidha, Kimario alisema kuwa Marie Stopes Tanzania ni shirika lisilo la kiserikali linalojishugulisha na afya hasusani ya uzazi, ambalo limekuwa likishirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto.

Ofisa Mawasiliano wa Marie Stopes, Ester Shedafa, alisema ili kuendana na uamuzi wa serikali katika sekta ya afya wamepanua wigo kwa kuweka namba za simu ili mwananchi apige bure na kuweza kupata huduma.

"Tumeongeza wigo kwa upande wa wataalamu tunategemea kuwa na daktari bingwa wa watoto na akina mama, ambao watatoa huduma ikiwamo afya ya uzazi, kliniki ya akina mama na watoto, vipimo vya Ultra sound, vipimo vya maabara, uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi, matibabu ya saratani ya mlango wa kizazi na chanjo ya homa ya Ini," alisema Shedafa.

Kwa upande wake, Kaimu Mganga Mkuu wa Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza, Nyaganyi Finias, alisema ni vyema jamii ikachukuwa hatua mapema ili kuepukana na athari za magonjwa, hususani saratani ya mlango wa kizazi ambao unazuilika iwapo mwanamke akifanyiwa uchunguzi mapema ili kubaini mabadiliko ya awali ya saratani.

"Tunaomba wananchi mjitokeze kujua afya zenu, Marie stopes wamechukuwa jukumu la kuiunga mkono serikali yetu kwa kujali afya za Watanzania, basi na sisi tujithamini ili tujue hali ya miili yetu kwa kufika hapa kwenye kituko hiki ili kupima na kuitambua afya yako, hii itasaidia sana kupunguza vifo vinavyoweza kuepukika," alisema Finias.

# RC Njombe ahimiza chanjo ya corona

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Marwa Rubirya, amewataka wananchi kuchukua tahadhari na kujikinga dhidi ya ugonjwa UVIKO-19 sambamba na kujitokeza kupata chanjo.

Alitoa wito huo kwenye uzinduzi wa Tamasha la Njombe ya Mama Samia lililoandaliwa na ofisi ya mkuu wa wilaya katika viwanja vya stendi ya zamani mjini humo.

Rubirwa alisema katika hospitali za mkoa huo, wagonjwa wapo, hivyo ipo haja ya kuchanja ili kujiondoa katika hatari.

"Ni kweli ugonjwa bado upo na katika hospitali zetu hapa mkoani tunao wenzetu ambao wanayo changamoto... na serikali inaendelea kuwahudumia, lakini niseme tunao wajibu wa kuhakikisha kuwa tunaendelea kuchukua tahadhari kama tunavyoelekezwa na wataalamu wa afya," alisema Rubirya.

Aliwahamasisha wananchi kupata chanjo hiyo kwa kusema: "Nawahamasisha wananchi ambao hawajachanja, twende tukachanje, tusiwasikilize wapotoshaji, tuwapuuze kwa sababu hao wengine wanaotupotosha huwezi kujua wengine wamekwishachanja.

"Tulizindua chanjo mwezi wa nane hapa mkoani, na mimi nilikua ni miongoni waliochanja siku ile, nilizindua zoezi hilo na viongozi wengi walishiriki na tunaendelea tukiwa na afya njema."

Rubirya alisisiza kwamba chanjo hiyo ni salama kwa sababu hata Rais alishaeleza, na kwamba hakuna kiongozi wa nchi anayeweza kuleta chanjo inayoangamiza wananchi wake.

"Sasa akishawaua ataongoza nini? kwa hiyo ni maneno ya upotoshaji tusiwasikilize kama alivyosema DC (mkuu wa wilaya) twende tukachanje, ujanja ni kuchanja," alisema Rubirya.

Mbunge wa Njombe Mjini, Deo Mwanyika, alisema chanjo ni hiyari, lakini Rais Samia alishaonyesha njia kwa sababu wengi walikua wanababaika.

"Wengi tulikua tunababaika, nina wasihi kama mbunge wenu ujanja ni kuchanja, tunahitaji tuwe salama na dunia imeshaonyesha kuna propaganda kubwa sana... nyingi katika jambo hili, propaganda zimeshaanza kuonekana ni za uongo," alisema Mwanyika.

"Wanasema watu wanakufa kwa sababu ya kuchanja, si kweli mbona ni miezi zaidi ya mitano nimechanja ninaendelea vizuri na ninadunda, mbona maambukizi yanazidi kupungua. hata wagonjwa mahututi wamepungua.. yote ni kwa sababu ya chanjo," aliongeza Mwanyika.

Awali mkuu wa Wilaya ya Njombe Kissa Kasongwa alimueleza mkuu wa mkoa kuwa Tamasha hilo litafanyika siku tatu likiwa na dhima nne ambazo ni utoaji wa huduma za kisheria, uhamasishaji wa chanjo ya corona ikiwa na kauli mbiu 'ujanja ni kuchanja', kutangaza utalii wa Wilaya ya Njombe na la nne ni kumshukuru Rais Samia kwa fedha nyingi ambazo amezipeleka katika wilaya hiyo.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba (kushoto), akizungumza na wafanyakazi wa kampuni ya Vodacom Tanzania, wakati alipotembelea banda la kampuni hiyo wakati wa kilele cha Wiki ya Huduma za Kifedha, katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Wa pili kulia ni Meneja Uhusiano wa kampuni hiyo, Alex Bitekeye na kulia ni Meneja Masoko wa M-Pesa, Noel Mazoya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Utouh: Uwazi muhimu uwajibikaji serikalini

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi isiyo ya kiserikali ya Wajibu, Ludovick Utouh, amesema bila kuwapo kwa uwazi katika utendaji wa serikali, uwajibikaji hautokuwapo.

Utouh ambaye ni Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) mstaafu, amesema ili uwajibikaji uwapo, ni lazima kwanza utanguliwe na uwazi, baada ya kuwapo kwa uwazi kwa kila mtu kujua kila kinachofanyika, watendaji watajikuta wanalazimika kuwajibika maana kila kitu kitakuwa kiko wazi.

Utouh ameyasema hayo, jijini Dodoma katika mahojiano alipokuwa akilitambulisha kongamano la kimataifa la ITAC, kujadili umuhimu wa uwazi na uwajibikaji katika kusukuma mbele maendeleo ya bara lote la Afrika.

Utouh alisema kongamano hilo la siku mbili, linafanyikia jijini Arusha kuanzia leo na kumalizika kesho, ambapo mada mbalimbali kuhusu umuhimu wa uwazi na uwajibikaji, zitawasilishwa na wataalamu wabobevu wa kimataifa kutoka Tanzania, Afrika na kimataifa.

Utouh alisema kongamano hilo lina umuhimu wa kipekee, kwa sababu bila kuwa na uwazi katika utendaji kazi serikalini, utendaji hautakuwapo, na kusisitiza, hoja za uhitaji wa serikali kutenda kazi kwa uwazi, ni takwa la kikatiba, na lipo kwenye Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977.

Jumla ya washiriki 500 kutoka sehemu mbalimbali, wanatarajiwa kushiriki kongamano hilo, ambalo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

# DC azuia wakazi kisiwani kuzaliana ovyo

**Na Richard Makore,** MAGU

MKUU wa Wilaya ya Magu mkoani Mwanza, Salum Kali, amepiga marufuku wakazi wa kisiwa cha Ijinga kilichoko ndani ya Ziwa Victoria kuzaliana bila utaratibu kwa kuwa hali hiyo itasababisha wakose eneo la kuishi.

Wakazi hao wapatao 2,800 wanaishi katika eneo lenye upana wa kilomita 8, na wanadaiwa kuzaliana kwa wingi kutokana na matumizi ya samaki aina ya ngele ambaye anachangia kuwapa hamu ya kujamiiana.

Mkuu huyo wa wilaya, alisema lazima kuwe na utaratibu maalum wa kuzaliana, na kwamba bila kufanya hivyo kisiwa hicho kitajaa watu na watakosa maeneo ya kulima na kujenga.

Akizungumza na wananchi wa kisiwa hicho, katika uzinduzi wa tenki la maji lililojengwa kwa ufadhili wa Meya wa Jiji la Wurzburg, Kali alisema eneo hilo ni dogo na kwamba lazima kuwe na utaratibu la kuongeza idadi ya watu ili kuendana na nalo.

Alisema kijiji hicho ambacho kipo kisiwani, kimepitia wakati mgumu kwa muda mrefu kwa kukosa maji safi na salama na kwamba msaada huo umekuwa mkombozi kwao.

Aliwataka wananchi hao kutunza mradi huo wa maji ambao umegharimu Sh. milioni 275 ambao una uwezo wa kusambaza maji katika vijiji sita katika kisiwa hicho.

Aliongeza kuwa kipindi cha nyuma wananchi wengi waliugua ugonjwa wa kichocho kutokana na kukosa maji safi na salama kwa ajili ya matumizi na kwamba kwa sasa tatizo hilo litabaki kuwa historia.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa mradi huo wa maji, Meya wa jiji la Wurzburg nchini Ujerumani, Christian Schuchardt, alisema gharama za mradi huo zinafikia Sh. milioni 275.

Alisema fedha hizo ni michango ya wananchi wa jiji hilo nchini mwake ambazo zilichangwa ili kunusuru afya za Watanzania.

Aliwataka wananchi hao kutunza mradi huo ili uendelee kuwasaidia katika kupata maji safi na salama katika kipindi chote.

Meya huyo aliyekuwa ameambatana na ujumbe wake kutoka Ujerumani, alisema wakazi wa eneo hilo kwa kipindi kirefu walikuwa wakisumbuliwa na ugonjwa wa kichocho kutokana na kunywa maji ya ziwa yasiyo salama.




Meneja Mwandamizi wa Chapa ya Coca-Cola Tanzania, Kabula Nshimo (kulia), akizungumza na baadhi ya wafanyakazi wa kampuni hiyo, jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu uzinduzi wa kampeni inayojulikana kama 'Maajabu Halisi na Coca-Cola' au 'Real Magic', unaotarajiwa kufanyika katika mikoa tofauti hapa nchini na kuendelea katika msimu wote wa sikukuu mpaka mwisho wa mwaka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CWT yataka vikao kutatua shida za walimu

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT) wilayani Sumbawanga mkoani Rukwa, kimewataka wawakilishi wake mahali pa kazi kuhakikisha wanafanya vikao vya kikatiba na wanachama, kwani ndio fursa ya walimu kukutana na kujadili changamoto na njia ya kuzitatua.

Mwenyekiti wa CWT wilayani Sumbawanga, Doseph Ndalama, aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua kikao cha siku moja cha wawakilishi mahali pa kazi kilichofanyika mjini Sumbawanga.

Alisema kuwa kwa muda mrefu, baadhi ya viongozi ambao ni wawakilishi mahali pa kazi hawaitishi vikao katika maeneo yao, kitendo kinawanyima fursa walimu katika maeneo waliopo kukutana na kutafutia ufumbuzi wa changamoto zao.

"Nawaagiza hakikisheni mnafanya vikao vilivyopo vya kikanuni na kikatiba, kwani hii ndio fursa ya awali kabisa kwa walimu kuanza kutatua changamoto zinazo wakabili, walimu wana matatizo mengi ambayo yanapaswa kushughulikiwa na CWT lazima mkutane na kuyafanyia kazi," alisema.

Katibu wa CWT Wilaya Sumbawanga, Peter Simwanza, aliwaambia walimu hao kuhakikisha wanakuwa bega kwa bega na chama chao, kwani kipo kwa ajili ya kuwasaidia kutatua changamoto likiwamo suala la maslahi kutokana na kuwa na madai ya msingi, ambayo yanapaswa kufanyiwa kazi na mwajiri.

Mmoja wa wajumbe wa kikao hicho, Mwalimu Vaileth Benedict, aliishukuru CWT kwa kuitisha kikao hicho kwani kimewapa fursa ya kuwakumbusha wajibu wao Sambamba na kuamsha ari ya utendaji kazi.

# TBL, UNITA zajitosa usalama barabarani

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia Tanzania (TBL) imezindua programu ya simu (App) ya usalama barabarani, kwa kushirikiana na Taasisi ya Mafunzo na Utafiti ya Umoja wa Mataifa (UNITAR), ambayo ilifanyika jijini Dar es Salaam.

Uzinduzi wa Programu hiyo ya simu ulikwenda sambamba na mafunzo ya usalama wa barabarani yaliyohusisha maofisa 15 wa Polisi kutoka kikosi cha usalama barabarani.

Mkurugenzi Mtendaji wa TBL, Jose Moran, alisema TBL inajivunia kushirikiana na UNITAR kuzindua programu hiyo ya simu, na itaendelea kushiriki katika mchakato wa kuboresha usalama barabarani Tanzania, ikizingatiwa kuwa suala hili ni muhimu katika kila nyanja ya maisha ya kila siku na pia ni muhimu katika ujenzi wa miji na jamii endelevu.

Programu hiyo ya simu(App) Management Practices for Safer Roads Toolkit iliyoandaliwa na UNITAR, ni mahsusi katika masuala ya usalama barabarani, itakayotumiwa na Polisi wa Tanzania.

Programu hii ni sehemu ya mpango wa UNITAR wa Mafunzo ya Kimataifa ya Usalama Barabarani (SDG), ambao unawianishwa na Mpango wa Kimataifa wa Muongo wa Utekelezaji wa Usalama Barabarani wa 2021-2030, ambao utasaidia nchi kufikia malengo ya utendaji wa Usalama Barabarani Duniani na unalenga kuchangia kufanikisha malengo ya SDG katika nyanja za afya na ustawi, miji na jamii endelevu na ushirikiano wa kimataifa kwa maendeleo endelevu.

Mafunzo hayo ya siku tatu yalijikita katika utumiaji wa mwongozo wa usimamiaji wa usalama barabarani wa UNITAR na utafiti mbili za majaribio zilizofanyika nchini Brazil na India na kuonyesha kuleta mafanikio.

Washiriki walichambua mwongozo kwa kujikita zaidi kuangalia jinsi ya kuboresha miundombinu ya barabara, umuhimu wa utekelezaji wa sheria, umuhimu wa kushirikisha wadau mbalimbali katika usalama barabarani, na wajibu wa kila mtu kama watumiaji wa barabara kuweka juhudi katika kuhakikisha matumizi ya barabara yanakuwa salama kwa watumiaji wote.

"Tumejitolea sana kuboresha usalama barabarani Tanzania mwaka mzima. Maofisa waliopata mafunzo walifurahishwa sana na fursa za mafunzo zinazotolewa na ushirikiano huu, na tunaiona kama mwelekeo sahihi wa kuchukua hatua muhimu, miundo na sera ili kuhakikisha kuwa ushirikiano unafikia malengo yaliyowekwa," alisema Angela Montano, mtaalamu wa mafunzo wa UNITAR.

# ama

AFYA NA MAZINGIRA

ALHAMISI NOVEMBA 18, 2021



Ukurasa 14

**TARI yatafiti na kuurejesha uwele, baada ndege washambulizi kuifilisi**



Ukurasa 13

Kukatisha dawa kunakuza ugonjwa akili, msururu wa madhara tofauti



Ukurasa 12

**MJADALA WA CHANJO CORONA**

**Hatua kwa kina zinavyotengenezwa na kauli ya usalama wake kutoka WHO**

# Wiki ya Magonjwa Yasiyoambukiza na darasa kuzuia hodi za maradhi mwilini

**Mwandishi Wetu,** ARUSHA

HADI wikiendi iliyopita, ilikuwa 'Wiki ya Magonjwa Yasiyoambukiza', ambayo kitaifa ilikuwa mkoani Arusha, ikilenga kuelimisha jamii namna ya kuyaepuka na hata njia za kukabiliana nayo.

Wadau wake Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza Tanzania (TANCDA), inayaainisha magonjwa hayo kuwa ni pamoja na; kisukari, moyo, mishipa ya damu, maradhi sugu ya njia ya hewa, matatizo ya akili, meno, saratani na yale ya kurithi kama vile siko seli.

Kuanzia alfajiri saa 12 asubuhi ya siku ya kwanza jijini hapa, watu walimiminika katika eneo la Gymkhana, kwenye uwanja maarufu wa Mgambo, tayari kwa matembezi maalumu ya ukakamavu.

Kila anayefika moja kwa moja anaanza mazoezi mepesi kupasha mwili joto, kabla ya kuanza rasmi ya matembezi maalumu, wakiongozwa na Mtaalamu wa Mazoezi Nchini, Waziri Ndonde na kaulimbiu ya mwaka ni 'Badili Mtindo wa Maisha Boresha Afya.'

Matembezi yanaanza kwa msururu mkubwa uliopitia katika viunga vya jiji la Arusha yakiwa na kila aina ya mbwembwe na vifijo vilivyotokana na baadhi ya watembeaji walionekana kupandwa na mori.

Magari mengi kwenye mitaa yanakopita matembezi hayo yanasimamishwa na Polisi wa Usalama Barabarani waliotanda kwenye maeneo ya matembezi, hata kunikumbusha nyakati wanafunzi walikuwa wanakimbia mchakamchaka asubuhi, wakipiga ngoma ili kujijengea ukakamavu.

Yanakatiza mitaa ya Impala Phillips, Mount Meru, Elbouru, Sanawari, Barabara ya Moshi, Mianzini na kumalizikia Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, yanapokewa na mgeni rasmi, Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Pauline Gekul.

Pia ameandamana na Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wzaee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, pia kuna mwenyeji wao Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela.

Gekul anawasifu washiriki wa matembezi, akiwataka wajenge utamaduni wa mazoezi, ikiwa njia ya kujikinga na kukabiliana na magonjwa yasiyoambuzika, akiwataka viongozi wa kada mbalimbali nchini nao kuhamasisha ufanyaji mazoezi katika maeneo yao ya kazi.

"Wafanyakazi wa serikali wapo hatarini kuugua magonjwa yasiyoambukiza, kutokana na kutumia muda mrefu kufanya kazi ofisini," anaonya na kuongeza kuwa, wakati wa kwenda na kutoka ofisini hutumia magari.

Gekul anawatahadharisha watumishi wasiofanya mazoezi kila mara, wanaingia katika hatari ya magonjwa yasiyoambukiza.

Naibu Waziri anakumbusha kuwa asiyefanya mazoezi na anakula mara tatu kwa siku, anajiweka hatarini kiafya kwa sababu lishe hiyo haitumiki yote, ziada inajirundika mwilini, hata kuwa chanzo cha magonjwa yasiyoambukiza kama shinikizo la damu, matatizo ya moyo, kisukari, saratani na uzito uliopitiliza.

Anasema, mazoezi yanaufanya mwili kutumia chakula cha ziada na kuwa mkakamavu, hata kuwa mbali na magonjwa yasiyoambukiza.

Gekul anawahamasisha wananchi kuamka mapema, pia kuacha tabia zinazokaribisha maradhi kama vile

kutofanya mazoezi, kula vyakula vyenye wingi wa mafuta, sukari na chumvi, kutumia tumbaku, dawa za kulevya na unywaji pombe uliokithiri.

Anarejea takwimu za magonjwa yasiyoambukiza zinaonyesha kuchangia vifo vya watu milioni 41 kila mwaka duniani, sawa asilimia 75 ya vifo vyote.

"Magonjwa haya siyo tishio tu ulimwenguni, bali hata hapa Tanzania. Hapa nchini katika miaka ya 60 magonjwa haya yalikuwa yanasababisha vifo asilimia 20, lakini kwa sasa yanachangia zaidi ya asilimia 33 hadi 40 kwa baadhi ya mikoa," anaonya.

Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Tiba, Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Timothy Wonanji, anasema kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wameandaa Mpango wa Kitaifa wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa hayo.

Mwongozo huo uliopo rasmi kwenye kitabu, anasema utasambazwa kitaifa ili watu wajifunze na kuepuka magonjwa hayo, ikiaminika kwa kiasi kikubwa utawasaidia wananchi kuepukana na vihatarishi vya magonjwa vinavyotokana na tabia, pia mtindo wa maisha.

Hapo anaorodhesha baadhi ya viashiria; ulevi wa pombe na kutumia tumbaku, kutofanya mazoezi na kutozingatia mlo kamili.

Njia pekee na rahisi ya kufikia malengo hayo, wataalamu hawa wanashauri kuwa ni jamii kubadili mtindo wa maisha na kuboresha afya zao, kuzingatia mazoezi ya mwili, mlo kamili, kuepuka matumizi ya tumbaku na kupunguza vyakula vyenye mafuta mengi, sukari na chumvi.

Mengine ni kuacha unywaji pombe uliokithiri, kutenga maeneo ya kufanyia mazoezi na wanaofanya kazi za ofisini kujitenge muda wa mazoezi.



Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Godwin Mollel (mwenye traksuti nyeupe), akiteta jambo na washiriki katika mazoezi kwenye Uwanja wa Mgambo, ikiwa ni Wiki ya Magonjwa Yasiyoambukiza kitaifa jijini Arusha. **PICHA: MTANDAO**

AFYA

MJADALA WA CHANJO CORONA

# Hatua kwa kina zinavyotengenezwa na kauli ya usalama wake kutoka WHO

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI dunia inahaha kuhakikisha chanjo iliyokwishapatikana dhidi ya maradhi ya corona inasambazwa duniani, Shirika la Afya Duniani (WHO), lina ufafanuzi wa undani wake unavyotengenezwa.

Kimsingi, chanjo inaundwa na vipande vidogo na chembe za ujumbe zinazosababisha magonjwa, sambamba na viungo vingine vinavyosaidia chanjo kuleta ufanisi.

Viungo vingi kila kimoja kinatumika kwa kusudi maalum. Hapo, kila kimoja hujaribiwa katika mchakato wa utengenezaji na inafanyiwa majaribio kwa sababu za usalama. Vifahamu viungo hivyo:

Antigeni: Kimsingi inasaidia kinga mwilini dhidi ya magonjwa. Inaundwa na sehemu ndogo ya viumbe vinavyosababisha magonjwa (bakteria, virusi, 'pollen') dhidi ya hitaji kama protini au sukari.

Vihifadhi: Inazuia chanjo kuharibika au kuchafuliwa baada ya kufunguliwa kizibo. Pale itatumika kuchanja mtu zaidi ya mmoja.

Zingine hazina hifadhi kwa sababu zinawekwa kwenye kasha ya dozi au kipimo kwa ajili ya mtu mmoja na inatupwa baada ya chanjo kutumika.

Vidhibiti: Kemikali kutoka machoni inayoweza kuwa sukari, tindikali amino na protini mwilini mwa binadamu, inayotokana na hamira au chachu.

Surfactants: Chembe inayoweka viungo vyote kwenye chanjo na inasaidia kutulia, au vitu vilivyoko kwenye mfumo wa maji kutogongana. Pia, hutumika katika vyakula kama barafu.


Mabaki; ni kiasi kidogo cha vitu vinavyotumika kutengeneza au huzalisha chanjo ambazo sio viungo hai katika chanjo iliyokamilishwa.

Vitu vinatofautiana kulingana na mchakato wa utengenezaji uliotumika na vinaweza kujumuisha protini za mayai, hamira au viuatilifu na athari za mabaki hayo, inatajwa kuwa ndogo sana mwilini.

Diluent-kimiminika; ni maji yanayotumika kulainisha chanjo katika usahihi unaohitajika kabla ya matumizi. Kimiminika kinachotumiwa zaidi ni majisafi.

Adjuvant-visaidizi; aina ya visaidizi vinavyoimarisha kinga kuhimili chanjo na kuifanya sindano ya chanjo ikae mwilini muda mrefu au kuamsha chembe za kinga.

Visaidizi hivyo, pia vinaweza kuwa vya kiwango kidogo cha chumvi chenye mjumuiko wa kemikali kama vile 'aluminium phosphate.'



Nyenzo ya chanjo inavyofanya kazi. **PICHA: MTANDAO**

> Chanjo lazima ithibitishwe kuwa salama na yenye ufanisi kwa watu wengi, kabla ya kuidhinishwa na kuingizwa kwenye programu za kitaifa za chanjo.

## INAVYOTENGENEZWA

Kila chanjo ni lazima ipitie majaribio ya kina, kuhakikisha usalama kabla haijaanza kutumika rasmi.

Inafanyiwa uchunguzi kubaini namna itakavyotumika kuamsha kinga, kisha inajaribiwa kwa wanyama, kutathmini usalama wake na uwezo wa kuzuia magonjwa na inapoleta mwitikio, ndio inafuata awamu ya kujaribiwa kwa binadamu katika awamu kuu tatu:

Mosi; chanjo hutolewa kwa idadi ndogo ya watu waliojitolea kuthibitisha ubora wake na kupata kipimo sahihi, ikihusisha vijana na watu wazima wenye afya njema.

Pili; Chanjo inatolewa kwa umma uliojitolea kutathmini zaidi usalama na uwezo wake kujenga kinga. Washiriki hapo wanakuwa na sifa sawa kama vile umri, jinsia, kulingana na walivyokusudiwa. Majaribio hayo ni ya kutathmini makundi ya umri na vigezo vingine vyo. Kundi ambalo halikupata chanjo, kwa kawaida hujumuishwa katika awamu hiyo ikiwa na kikundi linganishi ambacho hakijachanjwa, kubaini mabadiliko.

Tatu: Kuna kundi kubwa zaidi hata idadi ya maelfu waliojitolea, wakilinganishwa na kundi kama hilo la wasiopata chanjo. Muhimu ni kubaini usalama wa chanjo tajwa. Majaribio mengine ya awamu ya tatu hufanywa katika nchi tofauti na sehemu nyingi za nchi husika, ili kupata uhakika wa utendaji wa chanjo hiyo kwa umma.

Kimsingi, majaribio ya awamu ya pili na tatu ya waliojitolea na wanasayansi wanaoendesha utafiti, hufichwa kujua na kupata uhalisia wa kina, ikipewa msamiati "kupofusha."

## INAVYOSHUGHULIKIWA

Baada ya majaribio na matokeo yote kukamilika, waliojitolea na wanasayansi walioendesha majaribio wanaarifiwa ni nani aliyepata chanjo hiyo.

Maofisa katika kila nchi hutathmini kwa kina takwimu za majaribio na kuamua ama waidhinishe chanjo hiyo kwa matumizi au la.

Chanjo lazima ithibitishwe kuwa salama na yenye ufanisi kwa watu wengi, kabla ya kuidhinishwa na kuingizwa kwenye programu za kitaifa za chanjo.

Baada ya hapo, ufuatiliaji zaidi unafanyika kukitumika mifumo sahihi ya usalama na ufanisi wa chanjo zote, hata kuwezesha wanasayansi nao kuwa na ufuatiliaji wao, wakitathmini kiwango kinachotumiwa na jamii ngazi ya juu au kidogo.

Takwimu hizo hutumiwa kurekebisha sera za matumizi ya chanjo, ili kuongeza athari zilizopo, pia kuruhusu chanjo kufuatiliwa kwa usalama kupitia wakati wote wa matumizi yake.

Wakati chanjo inapoanza kutumika, ni lazima ifuatiliwe kila wakati kuhakikisha inadumu kuwa salama.

## VITA VYA CORONA

Mnamo Machi mwaka huu, WHO ilitangaza hakuna sababu ya kusitisha matumizi ya chanjo ya AstraZeneca, kwa kuhofia madai yanayotolewa kama vile kuganda damu ya mhusika, kwa kukosa ukweli unaohusiana madai hayo yanayosambaa.

Ni taarifa kwa mataifa kama Bulgaria, Denmark na Norway zilisitisha matumizi ya chanjo hiyo, kama ilivyo kwa Thailand, Italia na Austria zilizositisha kwa tahadhari.

WHO inahimiza hakuna uhusiano kati ya chanjo hiyo na hatari ya damu kuganda na mtaalamu wake, Dk. Margaret Harris, anaitetea chanjo ni salama na iendelee kutumika, akifafanua imeshawafikia watu milioni tano barani Ulaya, hadi miezi nane iliyopita.

Kulikuwapo madai ya watu 30 barani Ulaya kupata madhara ya kuganda damu, ikiainishwa na kifo cha mama mwenye miaka 50, baada ya chanjo.

WHO inatamka kuendelea na uchunguzi dhidi ya madai hayo, ingawa Dk. Harris anasisitiza hakuna uhusiano wowote na matatizo ya kiafya yaliyoripotiwa.

Mataifa ya Bulgaria, Denmark, Iceland ziliacha kuendelea na dozi ya kinga, pia Norway, Thailand, Italia na Austria zilichukua hatua kama hiyo kwa tahadhari.

Shirika la Dawa la Muungano wa Ulaya (EMA), lilisema awali hakukuwapo dalili za chanjo hiyo kusababisha kuganda damu mwilini, ikihimiza faida zake ni kubwa kuliko hatari zake."

Pia kunaelezwa kufanyika utafiti mkubwa katika majaribio ya tiba katika maabara za Ureno, Australia, Mexico na Ufilipino, wanakoendelea na mpango wa utoaji chanjo.

Mataifa mengine ambayo yanaendelea kutoa chanjo hiyo ni Uingereza, Ujerumani, Mexico na Australia.

## HAKUNA USHAHIDI

Nchini Uingereza, Shirika la Udhibiti wa Bidhaa za Huduma za Afya (MHRA), limesema hakuna ushahidi wa kuwapo chanjo iliyosababisha matatizo na watu wanapaswa kuendelea kuchanjwa wanapoombwa kufanya hivyo.

Zaidi ya dozi milioni 11 za chanjo ya AstraZeneca zimekwishatolewa Uingereza kwa mujibu wa MHRA, huku Ureno inasema faida za chanjo zinaendelea kuwa kubwa kuliko athari zake kwa wagonjwa.

## INAVYOFANYA KAZI

Chanjo ya AstraZeneca iliyotengenezwa na Chuo Kikuu Oxford, Uingereza kutokana na virusi vinavyosababisha mafua ya kawaida iliyodhoofishwa, inafahamika kwa jina 'adenovirus' kutokana na sokwe.

Ni virusi vilivyobadilishwa umbo vikaonekana zaidi mithili ya corona, ingawa haviwezi kusababisha ugonjwa. Mtu anapochomwa chanjo hiyo, inaunda mfumo wa kinga mwilini, jinsi ya kupambana na virusi halisi, pale utakapohitaji kufanya hivyo.

AFYA

# Kukatisha dawa kunakuza ugonjwa akili, msururu wa madhara tofauti

**Dk. Raymond Mgeni**

MOJA ya shida kubwa katika magonjwa ya akili, ni mtu kupata hali tofauti ya uhalisia, mabadiliko ya kufikiri, kuhisi na kutenda.

Mabadiliko hayo yanapojitokeza yanaweza kumfanya mhusika mwenye shida ya akili, anaweza kuharibu vitu na kuwajeruhi, hata kudiriki madhara ya kupoteza maisha ya wanaomzunguka.

Mtu anapokuwa katika hali hiyo anakuwa tofauti hali inayoweza kumfanya alete madhara, pasipo kujua hatari iliyoko. Wapo waliochoma moto nyumba na wanapodadisiwa kulikoni hatua hiyo, hisia zinaangukia tafsiri tofauti kuhusu mali au nafsi ya mhusika, hata binafsi akidhani anajitetea dhidi ya mabaya yasiyokuwapo.

Hapo ndio kuna sababu za wagonjwa wengi wa akili kupelekwa vituo vya polisi, kupata kesi za jinai mfano kesi za mauaji kwa matendo kama hayo.

Matukio mengi ya kihalifu, mara nyingine yanahusisha watu ambao wamepata shida za akili, kukiwapo vyanzo mbalimbali, mathalan wapo ambao wametumia dawa za kulevya.

Ni aina ya watu katika fikra hizo potofu zitokanazo na athari tajwa, katika harakati za kukabiliana na kiu ya dawa ya kulevya (alosto) wanathibitika kupora, hata kufikia ngazi wanabomoa nyumba ili wapate fedha au vitu vya kuuza kukidhi mahitaji yao.

Kunapofanyika hilo, huwa kunawaacha wanaangukia kwenye mikono ya sheria kutumikia kesi za jinai.

Hali kadhalika, wapo wanaovunja sheria hali ya kuchanganyikiwa inapojitokeza ghafla au katika dalili za awali. Kwa wanaoanza ghafla, kuna kundi la wenye matatizo ya kifafa chenye kuchanganyikiwa.

Mtu anazirai na kisha anapozinduka kutoka kwenye degedege, huwa anaambatana na mabadiliko ya tabia. Kuchanganyikiwa kunakoendana na balaa la kuchukua hatua zenye matukio ya hatari, baadhi wanabeba vifaa hatari na kupiga wengine au anajijeruhi.

### DALILI ZA AWALI

Kuna dalili za awali zinazojitokeza na kutajwa kwa mwenye mwelekeo wa shida ya akili. Dalili za awali za jumla huwa anakosa usingizi, hasira zilizopitiliza, anazungumza visivyoeleweka, vipindi vya huzuni zilizopitiliza, kuzubaa, msahaulifu wa kuzungumza au kucheka bila ya sababu.

Ujumla wake kitaalamu, zinatoa ishara ya dalili za shida ya akili inayoendelea. Ni bahati mbaya wengi si wanaochukua hatua kuwahi matibabu, hivyo wanamuacha mtu anaendelea kuugua akili hadi anapopata mabadiliko ngazi ya tabia hatarishi.

Mfano hai, kuna suala la mtu kumpiga au kujeruhi mwenzake, huwa kuna nyakati hali hizo zinaweza kumfanya akaharibu vitu, kujeruhi mtu au hata kumuua. Matatizo hayo yanapojitokeza yana athari kufikia mkono wa sheria, maana unatoa nafasi ya kusikiliza upande wa pili waliopoteza ndugu zao au kuharibiwa vifaa.

Kuna kundi la tatu; wanaoanza matibabu ya akili, ila wameyaacha kwa sababu mbalimbali kama vile za kifedha, kuhisi wamepona, ushawishi wa ndugu kutafuta tiba mbadala au maudhi ya dawa.

Matibabu ya akili huchukua muda mrefu na hili linawafanya wengine wasiwe na ufuasi mzuri wa dawa hasa wanapohisi wamepona.

Hali ya ugonjwa hujirudia pindi mtu anapoacha dawa ya bila maelekezo sahihi kutoka kwa daktari. Hali inaporudia, huja na dalili za awali, ikiwamo tabia zenye madhara kama yaliyotajwa.



Maadhimisho mojawapo ya Siku ya Afya ya Akili Duniani. **PICHA ZOTE: MATANDAO**



Akiwa katika hisia kali.

> **Mwenye sonona hupitia vipindi vya huzuni, upweke, hatia na kujiona hana thamani kabisa, sasa akishikwa na mawazo ya kukatisha maisha.**

### TABIA HATARI

Mtu huenda asijue ni wakati gani anapatwa na hali hiyo, hata akatenda kinyume na sheria. Yapo matukio ya kujiua, baadhi yakihusianishwa na shida ya akili. Wapo wa makundi ya wagonjwa yenye majina ya kitaalamu: Sonona, kundi linaloongoza kujiua; wagonjwa wa Baipola; na Sikizofrenia.

Mwenye sonona hupitia vipindi vya huzuni, upweke, hatia na kujiona hana thamani kabisa, sasa akishikwa na mawazo ya kukatisha maisha.

Hali hiyo inapozidi wiki mbili au zaidi pasipo matibabu kuwapo hatua za kitabibu, kujiua kunakuwapo karibu sana.

Wagonjwa kutoka makundi ya Baipola na Sikizofrenia, kuna wakati wanajihisi wanasikia sauti ambazo kiuhalisia hazipo na zinaweza kambatana na kutoa maelekezo ya mtu ajiue.

Hapo ndipo hatari yake inachukua nafasi mtu mtu akiitikia hilo anajiua, ingawa mawazo yake nayo yakamtuma upande wa pili, anaweza kufanya matendo ya mauaji kwa wengine.

Ni hali ya kubadili uhalisia na akili ikiamini inachokifikiri ni moja ya matukio ambayo yapo naye katika kuichukulia hatua anangukia kudhuru kabisa.

Kwa mama anayetoka kujifungua na akachanganyikiwa akili, ana hatari ya kumdhuru mtoto endapo atamwona kwa tafsiri tofauti na uhalisia wa jamii.

Wapo wanaojikuta hata wakadhuru mtoto akimfananisha ameshika nyoka. Wakati mwingine mtu mwenye changamoto ya akili, anaweza kusikia sauti zinazomwamrisha kutenda matendo ya kuharibu au kudhuru wanaomzunguka akitawaliwa na hisia ni adui zake.

### UMUHIMU WA TIBA

Kunatajwa kuna umuhimu wa tiba ya awali, kwa mtu ambaye ameshaanza kupata dalili za magonjwa ya akili ambayo katika sura moja inayosaidia madhara kutoka kwa wahusika.

Jamii inapochangia kuwezesha kundi hilo kuwa na hitaji la msaada, ni mchango katika kupunguza idadi ya wagonjwa wa akili hata katikia mikono ya jinai kisheria.

***• Anapatikana kwa mawasiliano: Simu; +255 676 559 211 na barua-pepe: raymondpoet@yahoo.com Hospitali ya Rufani Kanda, Mbeya***

MAZINGIRA

# TARI yatafiti na kuurejesha uwele, baada ndege washambulizi kuifilisi

- Miaka mitatu maabara yatoa majibu
- Mbegu sugu 'isiyosikia' la mharibifu

**Na Elizabeth Zaya**

UWELE ni miongoni mwa mazao yanayolimwa Tanzania na kwa miaka mingi yamekuwa yakishambuliwa na ndege, hata kusababisha wakulima kukata tamaa kulima zao hilo.

Inaelezwa ndege hao washambulizi walianza kuonekana kuwa kikwazo kikubwa kinachokwamisha ustawi wa zao la uwele mkoani Dodoma, hata Kituo cha Utafiti wa Kilimo (TARI) kilichoko Hombolo, wakaamua kusaka majibu.

Ni aina ya usakaji mwarobaini sahihi wa kitaalamu kupambana na tatizo hilo linalochukua sura ya usugu, tayari TARI imeshabuni mbegu mpya ya uwele ambayo haishambuliwi na ndege waharibifu hao sasa, kama ilivyokuwa zamani.

Meneja wa TARI, Hombolo Dk. Lameck Makoye, anasema mbegu hiyo inatarajiwa kutolewa hivi karibuni kwa ajili ya matumizi kwa wakulima, akiwa na ufafanuzi ina manyoya magumu ambayo ndege hawana uwezo wa kuyashambulia.

"Kwa miaka ya hivi karibuni, kumekuwapo tatizo kubwa kwa zao la uwele kushambuliwa na ndege na hili limesababisha wakulima wengi kuogopa kulima, japokuwa ni miongoni mwa mazao muhimu yanayohitajika si kwa biashara tu hata kwa chakula.

"Ndio maana wakulima wengi kwa sasa wanaogopa kuilima wakihofia kupata hasara kutokana na tatizo hilo la kushambuliwa na ndege," anasema Dk. Makoye, akifafanua ni mbegu iliyofanyiwa utafiti kwa miaka mitatu.

Anafafanua: "Tunatarajia kwamba baada ya mbegu hii kuingizwa sokoni na kuanza kutumika, italeta tija kubwa hususani kwa upande wa uzalishaji. Mavuno yataongezeka na mbegu hii ina sifa za kuvumilia mazingira ya ukame.

"Pia, kwenye lishe ina virutubisho vingi, ina madini ya zinki, iron (chuma), maginisiam na casium kwa wingi na inasaidia kuongeza vitamini B, madini ya chuma, kwa hiyo mbali na kuwanufaisha wafanyabiashara, pia ina faida nyingi kwa wale wanaolitumia kwa masuala ya afya."

Waziri wa Kilimo, Profesa Adolf Mkenda, wakati anazindua Kituo cha Usambazaji Teknolojia za Kilimo kilichoko Nzuguni jijini Dodoma, mahsusi ikiwakilisha Kanda ya Kati, anasema tija ndogo ya kwenye mazao yanayozalishwa nchini, ni miongoni mwa yanayokwamisha uwekezaji kwenye viwanda.

Pia anataja ni mambo yanayochangia wakulima kushindwa kutumia mbinu bora za kilimo, ikiwamo kutotumia utafiti, huku wawekezaji wengi wanaogopa sekta ya viwanda, wakihofia uhaba wa mazao ya kilimo yanayokidhi mahitaji.

"Ukimwambia awekeze kwenye kiwanda kwa ajili ya alizeti, anakuuliza je, uzalishaji wake ukoje? Siyo naweka kiwanda halafu mwisho wa siku nakosa malighafi. Kwa hiyo, Tanzania bado tuna tatizo kubwa la kuongeza tija kwenye mazao yetu," anasema Waziri Mkenda.

> **Ukimwambia awekeze kwenye kiwanda kwa ajili ya alizeti, anakuuliza je, uzalishaji wake ukoje?**

### KILIMO CHA MAZOEA

Pia anataja lingine linalokwamisha maendeleo ya kilimo nchini ni wakulima kuendelea kuwajibika kwa mazoea, wakishindwa kutumia utafiti unaofanywa na TARI, kulima kisasa na kuinua sekta hiyo.

Anaisifu asasi hiyo kwa kufanya kazi kubwa ya kiutafiti kusaidia kuleta mapinduzi kwenye sekta ya kilimo, ingawa anawalamu wakulima wengi bado ni wazito kuitumia kuwasaidia kuongeza tija kwenye mazao yao.

"TARI imefanya kazi kubwa ya kitafiti kwa ajili ya kuinua sekta hii ya kilimo, lakini wakulima wanafanya uzembe kuitumia, bado wanalima kimazoea na hili siyo fumbo wanajua nini wanatakiwa kufanya, tuanze kutumia sasa utafiti unaotolewa na taasisi yetu hii ya utafiti wa kilimo," anasema Profesa Mkenda.

"Ninaamini kwamba wakulima wakianza kutumia utafiti huu wa TARI watakuwa wanazalisha mazao mengi, hata bei ya vyakula itakuwa chini lakini wakulima bado watapata kipato, hakuna atakayeumia, si mlaji wala mkulima."



Wataalamu wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo (TARI) kilichoko Hombolo, Mery Kiyaiya (kushoto) na Ernesta Sanga, wakishughulika kwenye shamba la majaribio. **PICHA: MTANDAO**

### BOSI WA HOMBOLO

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Geoffrey Mkamilo, anaahidi watahakikisha wanaendelea kufanya utafiti na kuibua suluhisho kwenye sekta ya kilimo.

Dk. Mkamilo Geoffrey anasema, vituo vilivyopo kwenye mikoa mbalimbali nchini, vinalenga kuwasaidia wakulima na ombi linalowaangukia ni kwamba wavitumie ipasavyo kubadilisha mfumo wao wa kilimo.

"Tunachowaomba wakulima wajenge utamaduni wa kutumia utafiti wa TARI, kwa sababu zinafanyika kwa ajili ya kuinua sekta hii ya kilimo na si jambo jingine. Upo utafiti mwingi karibu kwa kila zao ambazo wakizitumia watafika mbali na wataongeza tija," anasema.

"Kila siku mambo yanabadilika, wasikubali kuendelea kulima kwa mazoea. Siku hizi, utafiti ndio unatakiwa utumike zaidi kabla ya kuanza kulima zao lolote," anasena Dk. Mkamilo.

Anaendelea: "Wakijenga utamaduni wa kufanya hivi, watakiinua kilimo kwa kiwango cha juu sana na hata hizi changamoto za kupanda kwa gharama za vyakula mara kwa mara zitaisha na hata viwanda sasa vitaongezeka sana."

### KAZI YA TARI

Dk. Mkamilo anasema TARI iliyoko chini ya Wizara ya Kilimo, imeanzishwa kisheria mwaka 2016 na jukumu lake kubwa ni kutafiti kilimo, pia kusimamia shughuli za utafiti wa aina nyingine zote ama kutoka ndani au nje ya nchi, ikimtaka kila anayetaka kufanya utafiti kilimo, ni sharti imfahamu na ndio mtoaji kibali cha kazi hiyo.

Anafafanua, pia TARI inashughulika na uendelezaji mazao ya mafuta, ikiwamo michikichi, alizeti, ufuta na karanga, lakini kwa ujumla duniani anataja mchikichi kuchangia mafuta kwmengi zaidi na ndio inawekewa nguvu zaidi nchini.



## Masheikh waonywa kuhusu ndoa bandia

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SHEIKH wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, amesema masheikh, maimamu na walimu ambao watakaongundulika kufungisha ndoa kwa kutumia vyeti feki watabutuzwa kwenye vyombo vya sheria ikiwamo kuwaondoa kwenye nafasi zao.

Pia amesema masheikh, maimamu na walimu ngazi ya kata ambao wanaoshindwa kujitambua kwenye kazi yao wataondolewa kwenye nafasi zao.

Sheikh Rajabu alitoa onyo hilo alipokuwa akizungumza na viongozi hao wa ngazi mbalimbali kwenye semina ya kuwajengea uwezo iliyofanyika jijini hapa.

Alisema viongozi hao ambao watakaongundulika kwenda kinyume cha maagizo na Katiba ya Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) kuhusu kufungisha ndoa kwa kutumia vyeti badia, hawataonewa aibu, badala yake watachukuliwa hatua.

Alisema kuna baadhi ya walimu maimamu ambao si waaminifu kwenye nafasi zao kutokana na kujiingiza kwenye utapeli wa kufungisha ndoa kwa kutumia vyeti visivyotambuliwa na BAKWATA.

"Mimi kama kiongozi wenu wa BAKWATA mkoa kwa kushirikiana na wasaidizi wangu wa wilaya, kata na mitaa, kamwe hatutakubali kuona udhalilishaji huo ukifanyika wa kufungisha vyeti vya bandia kwenye hizo ndoa kwa sababu tu ya kutaka kujipatia umaarufu na vijihela," alisema.

Sheikh Rajabu aliwataka viongozi hao kuhakikisha wanaondokana na kufanya kazi zao kwa mazoea badala yake wajitathmini kwa kujiongeza kwa manufaa ya waislamu wanaowaongoza na kwa taifa pia.

Alisema, bado kuna baadhi ya viongozi wa BAKWATA kuanzia ngazi ya chini hadi mkoa, wanaofanya kazi zao kwa mazoea hawatavumiliwa na kama wanajitambua hivyo, wajiondoe kwa ajili ya faida ya uislamu na jamii inayowazunguka.

Akizungumza kwa niaba ya viongozi hao, mwalimu wa madrasa ya Muhajirina kata ya Chang'ombe, Ustadhi Yahaya Kivuma, aliiomba BAKWATA kuwajengea uwezo viongozi hao mara kwa mara ili kuondokana na kufanya kazi kwa mazoea.

# Kampeni elimu ya ardhi nyumba kwa nyumba

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

OFISI ya Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Dodoma kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dodoma, inafanya kampeni ya mtaa kwa mtaa kwa ajili ya kutoa elimu ya umiliki wa ardhi kwa wananchi.

Lengo la kampeni hiyo ni kukutana na wananchi kwenye maeneo yao na kuwapa tahadhari kuhusu ujenzi bila vibali ili kuepuka usumbufu wa kubomolewa nyumba zao.

Kampeni hiyo inaendeshwa kwa kuwapatia elimu kwa njia ya mazungumzo, matangazo, sanaa za maigizo, nyimbo za asili pamoja na kugawa vipeperushi vinavyoelezea masuala mbalimbali yanayohusu ardhi ikiwemo vibali vya ujenzi na kodi za pango la ardhi.

Aidha, kampeni hiyo imelenga kumfikishia mwananchi hususan mkazi wa Jiji la Dodoma elimu kuhusu umiliki wa ardhi, ujenzi kwa kufuata taratibu za mipango miji, kodi ya pango la ardhi na fursa mbalimbali zinazopatikana kwenye sekta hiyo ikiwamo viwanja vya makazi na uwekezaji wa viwanda.

Ofisa Habari wa Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Dodoma, Hassan Mabuye, alisema kampeni hiyo kwa awamu ya kwanza inafanyika kwa siku tano mfululizo.

Mabuye alisema suala la kuwafuata wananchi katika maeneo yao na kuwapatia elimu hiyo kuhusu masuala mbalimbali ya ardhi ni endelevu na hapo baadaye itafanyika katika wilaya zote za mkoa wa Dodoma.

"Mpaka sasa tumeshazunguka na kutoa elimu hii katika maeneo kadhaa ya jiji la Dodoma kama Ihumwa, Nzuguni, Chang'ombe, Nkuhungu, Majengo, Mnadani Swaswa, Ilazo, Kikuyu, Chidachi, Makulu na Mnada wa Kizota. Mwitikio ni mkubwa sana na bado tunaendelea katika maeneo mengine yote ya Mkoa wa Dodoma na tunatarajia kufika hadi vijijini," alisema Mabuye.

Alitoa wito kwa wakazi wa jiji la Dodoma kujitokeza kwa wingi pale ambapo kunafanyika mikutano hiyo katika maeneo yao ili kupata elimu hiyo.

Ofisa Habari wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Ramadhani Juma, alisema fursa ya jiji hilo ya kushirikiana na Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Dodoma inawasaidia kuwaelimisha wakazi wa jiji hilo kuhusu masuala ya ardhi.

Alisema pia itawasaidia kupunguza changamoto kadhaa za uelewa kwa wananchi kwani wanapata fursa pia ya kuuliza maswali kwa mambo yanayowatatiza.

"Lakini pia tunawatangazia uwepo wa fursa za upatikanaji wa viwanja vinavyouzwa na halmashauri kwa ajili ya matumizi mbalimbali katika maeneo ya jiji ikiwamo eneo maalum la uwekezaji wa viwanda kwenye Kata ya Nala. Tayari baadhi ya wawekezaji wameanza ujenzi wa viwanda kikiwamo cha mbolea ambacho kitakuwa kikubwa kwa Afrika Mashariki ambacho tayari ujenzi wake umeanza," alisema.

Pia Juma alisema katika mikutano hiyo na wananchi wanawakumbusha wale ambao walishanunua viwanja na bado hawajakamilisha malipo kufanya hivyo hadi kufikia Novemba 30, mwaka huu kwa kuwa baada ya hapo vitauzwa upya kwa wateja wengine.

Aliyataja baadhi ya maeneo ambayo wateja wengi hawajakamilisha malipo ya viwanja kuwa ni pamoja na Mtumba, Kikombo, Nzuguni, Iyumbu, Njedengwa, Michese, Mkalama, Nala, Michese, Wia, na Mahomanyika.




Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, akiwasilisha taarifa ya mafanikio na matatizo ya sekta ya viwanda na biashara kwenye mkutano na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Sekretarieti ya ajira yaingilia kati sakata la kughushi vyeti

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SEKRETARIETI ya Ajira imeahidi kushughulikia mfumo wa teknolojia ili kutatua na kubaini matatizo ya watu wanaoghushi vyeti ili wapate kazi.

Hayo yalibainishwa na Katibu wa Sekretareti ya Ajira, Xavier Daudi, wakati akizungumza na waandishi wa habari kabla ya uzinduzi wa bodi ya nne ya sekretarieti hiyo uliofanyika jijini Dodoma.

Daudi alisema sekretarieti imetakiwa kuongeza kanzidata kutoka shule ya msingi hadi vyuo ambazo zitasaidia kujua wahitimu wako wapi na wanafanya nini baada ya masomo yao.

Alisema wana changamoto hizo katika sekretarieti lakini watahakikisha wanakabiliana nazo ili mambo yote yaende sawa.

"Pamoja na mafanikio tuna changamoto mbalimbali zinatukabili za kughushi vyeti, kumbi za kufanyia usaili na zingine nyingi. Lakini tunajipanga kukabiliana nazo," alisema.

Alisema changamoto nyingine waliyo nayo ni pamoja na jamii kuamini kila mwanachuo anayemaliza ni lazima aajiriwe jambo ambalo linahitaji wapewe elimu ili kujua si wote ambao watapata ajira serikalini.

Kutokana na hali hiyo, alisema wataendelea kuwaelimisha jamii ili kujua wanapohitimu kuna vitu vingi vya kufanya na si kusubiri ajira pekee serikalini.

Hata hivyo, alisema wanajitahidi kutoa elimu kwa jamii ili ielewe nini inatakiwa kufanya baada ya kuhitimu masomo yao ya vyuo vikuu.

Kuhusu uboreshwaji wa mifumo ya teknolojia, alisema suala hilo watalifanyia kazi ili kuondoa kero ya kughushi vyeti ambayo inawakabili.

Alisema wako imara kuhakikisha haki inatendekea katika suala zima la utoaji ajira kama walivyoelekezwa na Wizara hivyo ametoa wasiwasi wananchi kuhusiana na suala hilo.

katibu huyo alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na kutoa vibali vya ajira katika sekta mbalimbali jambo ambalo litachagia kwa kiasi kikubwa katika utendaji kazi wa kila siku kwa wafanyakazi.

Alisema Rais Samia amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha wananchi hasa vijana wenye jamii wanapata ajira ili kukuza uchumi wa taifa na kuahidi kuwa hawatamuangusha watashirikiana naye kuhakikisha wanaajiri watu wenye weledi na ambao watakwenda kufanya kazi bila kikwazo chochote.





# Mgogoro KKKT Dayosisi ya Konde wamalizika

**Na Grace Mwakalinga,** TUKUYU

HATIMAYE mgogoro wa waumini na uongozi wa Kanisa la Kilutheri la Kiinjilisti Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Konde Juu ya kuhamishwa makao makuu kutoka Tukuyu kwenda Ruanda, jijini Mbeya umemalizika.

Mgogoro huo umemalizika baada ya Askofu wa Dayosisi hiyo, Dk. Edward Mwaikali, kukubali kurejesha makao makuu Tukuyu.

Uamuzi huo umefikiwa na kutolewa taarifa jana na Mkuu wa KKKT, Dk. Fredrick Shoo, kwenye kikao kilichofanyika mjini hapa kwa ajili ya kutafuta maridhiano.

Dk. Shoo katika taarifa hiyo alisema pamoja na kasoro zilizojitokeza za ukiukwaji wa sheria, kwa pamoja wamekubaliana makao makuu yabaki Tukuyu na kwamba Halmashauri Kuu ya Kanisa itaunda kamati ambayo itaitisha mkutano mkuu wa kujadili suala la wachungaji waliosimamishwa kutoa huduma.

"Tuko hapa kwa ajili ya kutafuta amani. Tunalipenda kanisa na waumini, hivyo tunapaswa kumwomba Mungu kujiepusha na migogoro ya kidini ambayo haimpendezi Mwenyezi Mungu," alisema Askofu Shoo huku akilaani kitendo kilichofanywa na waumini kumdhihaki Askofu Mwaikali.

Naye Askofu wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dk. Askofu Alex Malasusa, alikemea kitendo kilichofanywa na waumini wa kanisa hilo cha kumfukuza Askofu Mwaikali kwenye ibada Agosti 22, mwaka huu, na kuwataka kungana na kuwa kitu kimoja.

Alisema mgogoro huo usilete mtikisiko ambao umesababisha kuvuruga amani na kusababisha vyombo vya dola kulazimika kuimarisha ulinzi na kuwataka kuwa watulivu na kuitafuta amani.

Malasusa alisema migogoro ya kidini inapaswa kukemewa na waumini wawe wamoja katika kumtukuza Mungu na si kuibua malumbano na kutokuwa na imani na viongozi wa dini wanaowaongoza.

Kwa upande wake, Askofu Dk. Mwaikali aliwaomba radhi waumini wa kanisa hilo na kwamba linaloshindikana kwa wanadamu kwa Mungu halishindikani na atatekeleza maagizo na maelekezo ya Mkuu wa Kanisa.

Alisema uamuzi uliofanywa si jambo jepesi, hivyo ana kila sababu ya kuwaomba radhi waumini kwa yote yaliyojitokeza na kumwomba Mungu awasimamie kuendelea kusonga mbele. Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Urlich Matei, alisema baada ya kikao walichofanya kwa kushirikisha maaskofu wa kanisa hilo, waumini na watendaji wa serikali wamefikia hatua ya kutatua mgogoro na kukubali ifikapo Novemba 22, mwaka huu, kiti cha kanisa ambacho ni miongoni mwa mali za dayosisi ya Konde vinarejeshwa.

Agosti 22, mwaka huu, katika Kanisa la KKKT Usharika wa Tukuyu ambako ni kanisa kuu la Dayosisi, waumini wa kanisa hilo walifanya vurugu kwenye ibada kupinga Askofu Mwaikali kuhamishia mali za kanisa kupeleka Ruanda jijini Mbeya. Hatua hiyo ilisababisha Jeshi la Polisi kuingilia kati na kumtoa ndani ya kanisa.

Miongoni mwa sababu zilizofanya waumini kufanya vurugu ni pamoja na kumtuhumu Askofu Mwaikali kuhamisha mali za kanisa, matumizi mabaya ya madaraka na kuwatimua kazi wachungaji 17 pindi wanapomshauri.



Mhitimu wa Mafunzo ya ufundi wa simu za mikononi katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Upendo Lunda (kulia) akitoa ufafanuzi kwa Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua (kushoto) jana, kuhusu mafunzo hayo yalivyowasaidia kufanya kazi zao kwa weledi na kutambulika na kupewa leseni na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Kukatika umeme chanzo ukosefu maji

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jiji la Mbeya (UWSA) imesema kukatika kwa umeme mara kwa mara kumechangia uhaba wa maji katika baadhi ya maeneo.

Ofisa Uhusiano na Huduma kwa Wateja wa mamlaka hiyo, Neema Stanton, alisema hayo jana wakati akitoa ufafanuzi wa kukatika kwa umeme ambako kumeyakumba baadhi ya maeneo ya Jiji la Mbeya na kusababisha adha kwa wananchi.

Alisema uhaba huo umesababishwa na kukatika kwa umeme katika Jiji la Mbeya, hivyo kusababisha mitambo ya kusukuma maji kushindwa kufanya kazi na matokeo yake baadhi ya maeneo kukosa maji.

Kwa mujibu wa Stanton, licha ya kuwapo kwa shida hiyo, mamlaka inafanya kila linalowezekana kuhakikisha maeneo yote yanapata maji kwa wakati huku akiwakumbusha wateja kuwa na utamaduni wa kuhifadhi maji ya ziada kwenye matangi au vyombo.

"Kumekuwa na shida ya umeme katika baadhi ya maeneo ya Jiji la Mbeya hali ambayo pia imeathiri mifumo yetu ya utoaji wa huduma za maji ukizingatia kuwa vyanzo vyetu na matangi yanategemea mitambo inayotumia umeme," alisema.

Baadhi ya wakazi wa Jiji la Mbeya walisema uhaba wa maji umeathiri shughuli zao za kiuchumi badala ya kufanya kazi, wanatumia muda mwingi kutafuta huduma hiyo katika maeneo ya mbali.

Anita Mwangambaku, mkazi wa Iwambi, alisema katika eneo analoishi hajapata huduma ya maji kwa zaidi ya wiki mbili hali inayomlazimu kukodi mkokoteni kufuata maji maeneo mengine.

"Kuna wakati ninaacha shughuli zangu za kushona nguo na kuamua kwenda kutafuta maji ya kutumia nyumbani. Fedha kidogo ninazozipata kupitia shughuli zangu nampa mtu wa mkokoteni ili aniletee maji nyumbani kwa ajili ya kupikia na kuoga mimi na familia yangu," alisema Mwangambaku.

## RC aagiza uchunguzi wa ununuzi wa magari

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya, imeanza ufuatiliaji na kuchunguza watumishi wanaoagiza magari kutoka nchi mbalimbali kupitia Bandari ya Dar es Salaam katika kipindi hiki serikali imewekeza mabilioni kwenye miradi ya kimkakati.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema amelezimika kufanya hivyo ili kudhibiti ubadhirifu wa fedha zilizotolewa na serikali kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

"Kuna watumishi ambao wakiona fedha za miradi zinaletwa ndiyo wanaona ni sehemu ya kupigia na kuagiza magari. Sasa nimeagiza uchunguzi kufanyika juu ya uagizaji wa magari na ununuzi wa mahitaji kwenye miradi," alisema.

Pia aliwatahadharisha wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri na maofisa ununuzi kusimamia vyema matumizi ya fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya miradi ili wasije kuingia kwenye matatizo.

"Ndugu zangu fedha hizo ni za moto nami siwezi kukubali watendaji waliopewa dhamana kushindwa kuzisimamia na kwamba zikitumika ndivyo sivyo zitaondoka na vibarua vya watu," alisema.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Sabasaba, Ally Mbika, alisema utendaji wa serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan unaonyesha nuru kwa Watanzania na kwamba Sh. milioni 400 zilitolewa kwa ajili ya ukarabati wa shule kongwe ya kutwa ya sekondari ya Mbeya Day.

Naye mkazi wa Forest, Stella Joel, alisema wakati serikali inatekeleza miradi ya maendeleo, jamii inapaswa kujitolea nguvu kazi kushiriki ili kuwezesha kukamilika kwa wakati.

# Ushirikiano wa kamati Bunge waikosha SMZ

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ameipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge inayoshughulikia masuala ya Ukimwi, kifua kikuu, dawa za kulevya na magonjwa yasioambukiza kwa ushirikiano wake na Serikali ya Zanzibar.

Hemed alieleza hayo jana katika kikao maalum kilichowakutanisha wajumbe wa kamati hiyo waliofika ofisini kwake kwa lengo la kubadilishana naye mawazo.

Alieleza kuwa Serikali ya Zanzibar inafarijika kutokana na ushirikiano inaoupata kutoka kwa kamati hiyo, kwa ushirikiano wa pamoja na viongozi wake ambapo kwa kiasi kikubwa imesaidia kupambana na matumizi ya dawa za kulevya.

Alisema kutokana na Zanzibar kuwa nchi ya visiwa, imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya upitishaji wa dawa za kulevya, kutokana na uwapo wa bandari nyingi zisizokuwa rasmi, zinazotumiwa na wahalifu wa vitendo hivyo.

Aidha, Hemed alisema uingizwaji wa dawa za kulevya, umesababisha Zanzibar kuathiriwa kutokana na vijana kujiingiza katika wimbi hilo, hali inayosababisha kupoteza nguvu kazi ya taifa.

Alieleza kutokana na ukubwa wa jiografia ya Tanzania utaratibu wa kubadilishana taarifa kwa pande mbili hizo utasaidia kudhibiti uhalifu wa vitendo hivyo.

Hemed alisema serikali haitamwonea aibu kiongozi yeyote atakayebainika kujihusisha na vitendo vya dawa za kulevya, na kwamba kupitia kikao kijacho cha Baraza la Wawakilishi, inatarajia kufanya mabadiliko ya sheria ili kuipa meno zaidi ya kiutendaji Tume ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za kulevya Zanzibar.

Naye Mwenyekiti wa Kamati hiyo ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum, Fatma Hassan Taufiq, alisema kamati hiyo imeamua kufanya ziara yake Zanzibar kwa lengo la kujifunza hatua bora zilizochukuliwa na serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kukabiliana na masuala mbalimbali yanayohusiana na kamati hiyo.

Fatma aliishauri serikali kuangalia namna ya kuliratibu suala la magonjwa yasioambukiza kutokana na kuisababishia serikali kubeba gharama kubwa ya matibabu kutokana na magonjwa hayo. Kamati hiyo pia ilikutana na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, ambapo amesema ni muhimu kwa taasisi na mamlaka zote zenye jukumu la kupambana na dawa za kulevya Tanzania kujifunza na kutambua ujanja na mbinu tofauti zinazotumiwa na wahalifu hao ikiwa ni njia muhimu ya kushinda vita hivyo kwa pamoja.

Othman alisema wahalifu wa dawa za kulevya wamekuwa wakitumia mbinu na ujanja mkubwa, hivyo ni vyema taasisi hizo kutambua hilo na kufanya kazi kwa pamoja na karibu zaidi kati ya pande mbili hizo ili kushinda vita dhidi ya tatizo hilo nchini.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, akizungumza na wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge inayoshughulikia masuala ya UKIMWI, kifua kikuu, dawa za kulevya waliofika ofisini kwake, Vuga, jijini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## 'Kuna kasi katika kesi za udhalilishaji'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais (Katiba Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora), Haroun Ali Suleiman, amesema katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, wamefanikiwa kuongeza kasi ya upelelezi wa kesi za udhalilishaji wa kijinsia na kutolewa hukumu haraka, hivyo kurudisha imani ya wananchi kwa vyombo vya sheria.

Waziri huyo aliyasema hayo jana wakati akitoa tathmini ya mwaka mmoja ya uongozi wa Rais Dk. Mwinyi katika kutekeleza majukumu yake katika wizara hiyo.

Alisema jumla ya kesi za jinai 8,659 zimefunguliwa katika mahakama mbalimbali na kesi 6,110 zimetolewa uamuzi ambapo kwa upande wa kesi za udhalilishaji wa kijinsia ni 698 na kesi 55 zimepata hukumu mbalimbali.

Aliwataka wananchi kuongeza ushirikiano kwa mahakama ikiwamo kutoa ushahidi na kuachana na tabia ya muhali kwa kuficha matukio hayo katika ngazi za familia.

Ameongeza mafanikio hayo yanatokana na kuimarishwa kwa mahakama za Unguja na Pemba ikiwamo kuongeza idadi ya majaji Mahakama Kuu hadi kufikia wanane, wakati mahakimu wa mikoa wamefikia 33 na Mahakimu wa Wilaya ni 13.

Aidha, alisema mahakimu wa mahakama za mwanzo nane, makadhi tisa hatua ambayo imesaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza kasi ya kusikiliza mashauri mbalimbali ya wananchi katika mahakama.

Alieleza kuwa katika mwaka mmoja wizara yake imefanikiwa kuongeza ufanisi katika vyombo vya sheria kwa kuongeza idadi ya watendaji ikiwamo majaji na mahakimu kwa ajili ya kusikiliza mashauri kwa kasi kubwa sambamba na kuanzisha mahakama maalumu ya udhalilishaji wa kijinsia.

Suleiman alisema jengo la Mahakama Kuu lilioko Tunguu limekamilika ambapo linatazamiwa kufunguliwa Januari 12 mwakani katika sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema moja ya changamoto kubwa na sababu ya kuchelewa kusikilizwa kwa kesi nyingi kwa wakati ni ukosefu wa nafasi za kusikiliza kesi kwa majaji na mahakimu na vyumba za kusikiliza kesi hizo kwa kuwahusisha wananchi.

# Kikwazo vijana kukosa fursa za uongozi hiki

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KUKOSEKANA kwa mikakati na mifumo madhubuti ya kumwandaa kijana kielimu na kiuchumi, kunasababisha vijana wengi kushindwa kuzifikia fursa mbalimbali za uongozi.

Akizungumza jana alipokuwa akiwasilisha mada katika mafunzo ya kuwajengea uwezo vijana juu ya ushiriki na ushirikishwaji wa uongozi katika ngazi za maamuzi Dunga Wilaya ya Kati Unguja, mwanasheria kutoka Jumuiya ya Habari dhidi ya Dawa za Kulevya (ZAIADA), Thneyuu Mabrouk Hassan, alisema licha ya serikali na taasisi mbalimbali kuendelea na juhudi za kumkomboa kijana, bado mifumo iliyopo sasa kuanzia ngazi ya msingi hadi elimu ya juu haijamwezesha kujiandaa na kukabiliana na maisha.

Alisema hali hiyo inasababisha kuongeza kundi kubwa la vijana ambao hawana ajira.

Alisema kwamba bado idadi ya nafasi za uongozi kwa vijana ni ndogo hasa nafasi za maamuzi, ukilinganisha na makundi mengine, hivyo ni vyema kwa serikali na jamii kutoa msukumo kwa vijana ili kupiga hatua za maendeleo.

Vijana walioshiriki mafunzo huyo wamewashauri wenzao kuwa tayari na uzalendo wa kujitolea katika kuitumikia serikali yao ili kuaminiwa na kupewa nafasi za uongozi. Amos Yussuf Lemeja, alisema aliwataka vijana wenzake kutokata tamaa na maisha badala yake kuzigeuza changamoto kuwa ni fursa katika kufikiana uthubutu, utayari na uzalendo kufikia malengo yao.

Mafunzo hayo ya siku moja yaliyowashirikisha makundi ya vijana na wajane, yaliendeshwa na ZAJAGA na kufadhiliwa na Foundation for Civil Society.

# Waziri Mhagama mgeni rasmi kongamano la Malkia Ladies

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, anatarajia kuwa mgeni rasmi wa Kongamano la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi, litakalofanyika Jumamosi jijini Dar es Salaam.

Kongamano hilo lililoratibiwa na kikundi cha Malkia Ladies, litahusisha washiriki wanawake, na litafanyika kwa kaulimbiu ya 'Mwanamke ni Nguzo ya Uchumi, Amka Uwekeze,' huku likitumika kuzindua kikundi hicho, Kampuni ya Bima, ramani ya jengo la biashara (Malkia Woman Market Mall) na Chaneli ya YouTube (Malkia Ladies Tv).

Malkia Ladies ni Kikundi cha Kikoba chenye wajumbe 34, kilichosajiliwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), kwa lengo la kuwasaidia wanawake kupitia elimu ya fedha kwa maana ya uwekaji akiba na uwekezaji kwa maendeleo yao na familia zao.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Malkia Ladies Group, Charity Mwakalonge, alisema kongamano hilo linalenga kuwanoa wanawake juu ya namna bora ya kuanzisha na kuviendeleza vikundi kwa ustawi wa biashara na miradi wanayofanya na kuiendesha, ili vilete tija miongoni mwao.

"Sisi kwa mfano tuko wajumbe 34, ambako mzunguko wetu wa fedha kwa mwaka ni takribani Sh. milioni 250 na hii imetokana na kikundi chetu kuwa na nidhamu ya uwekaji akiba na kuanza uwekezaji kupitia fursa mbalimbali na ndipo tukaja na wazo la kongamano hili, ili kuwasaidia wanawake wengine.

"Tunawakaribisha wanawake wa Dar es Salaam na Tanzania kwa ujumla, kushiriki tamasha hilo litalofanyika kwa mfumo wa kongamano. Lengo ni kuwasaidia kujua namna sahihi ya kuanzisha na kuendeleza vikundi, pia tutachagua vikundi vitatu bora vitakavyoshiriki ambavyo kwa kuanzia tutavilea hadi vifikie kiwango kikubwa zaidi yetu.

Alifafanua kuwa pia watazindua kampuni ya bima itakayoanza kutoa huduma hivi karibuni, ramani ya jengo la maduka 100 ya wanawake kuuzia bidhaa zao, kitabu cha fursa 50, pamoja na Chaneli ya Malkia Ladies Tv ambayo itakuwa chachu ya kinamama kupata elimu ya masuala ya vikundi na uwekezaji, itakayotolewa kupitia mada na watoa mada tofauti, akiwamo Aunt Sadaka.

Husna Mkupete ambaye ni Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Jamii na Chevawe Mberesero, Mwenyekiti Kamati ya Uwekezaji, walitoa wito kwa wanawake mmoja mmoja ama vikundi kujitokeza kwa wingi Jumamosi, ili kupigwa msasa utakaowawezesha kutekeleza majukumu yao kibiashara na kijasiriamali kwa weledi na kukuza pato lao na vikundi vyao.




Mwenyekiti wa Malkia Ladies Group, Charity Mwakalonge (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kuwakaribisha wanawake kwenye tamasha la uzinduzi rasmi wa kikundi cha Malkia Ladie, litakalofanyika Ukumbi wa PTA Sabasaba, Barabara ya Kilwa Jumamosi. Kulia ni Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Jamii ya kikundi hicho, Husna Mkupete na Mwenyekiti Kamati ya Uwekezaji, Chevawe Mberesero. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kliniki maalum kutoa huduma za kibingwa Sekou Toure yaanza

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Mwanza, Sekou Toure imeandaa kliniki maalum ya huduma za kibingwa za uchunguzi wa magonjwa na matibabu kwa wagonjwa mbalimbali.

Huduma hizo zitakazotolewa kwa siku tano zinatarajia kuwafikia wananchi 2,500 mkoani Mwanza.

Akizungumza na waandishi wa habari kabla ya kuzinduliwa kwa kliniki hiyo, Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Bahati Msaki, alisema wananchi watapata huduma za uchunguzi na matibabu ya kibingwa kwa gharama nafuu na kwa siku watawafikia wagonjwa 500.

Alisema wameweka kiwango cha Sh. 10,000 ambacho ni nusu ya gharama za kumuona daktari ili kurahisisha na kutoa fursa kwa wananchi wengi kupata huduma hizo.

Alizitaja huduma hizo kuwa ni pamoja na upimaji wa magonjwa ya moyo, figo, macho, kisukari, homa ya ini, saratani ya matiti na mlango wa kizazi, upasuaji, mifupa, afya ya kinywa na meno.

Katika matibabu hayo, madaktari bingwa wa watoto na wanawake, upasuaji na magonjwa ya ndani watapatikana katika kipindi chote.

Alisema wameamua kuweka kambi hiyo maalum ili kupeleka huduma kwa wananchi kwa urahisi na kwa gharama nafuu itakayomsaidia mwananchi kumwona daktari bingwa na kupata huduma.

Aliongeza kuwa wameboresha maeneo mbalimbali ya hospitali, wamenunua dawa za kutosha, mashine za maabara na vipimo vya idara ya mionzi, ununuzi wa mashine za kupima magonjwa tofauti ili kuwasogezea wananchi huduma bora.

Aliwaomba wananchi wa Mwanza na mikoa jirani ya Kanda ya Ziwa kwenda kupata huduma hizo na kuwaomba wasiwacheleweshe wagonjwa wao kufika kupatiwa matibabu.

"Tulikaa na madaktari bingwa wenzangu tukaona tufanye zaidi ya kile tunachokifanya ili kuhakikisha jamii inapata huduma za kibingwa kwa karibu pia vipimo vingine kama kupima presha, kisukari, uzito, homa ya ini, saratani ya matiti, chanjo ya UVIKO-19 tumeamua kufanya bure kuanzia Novemba 15 hadi 19," alisema.

Akizindua kambi hiyo ya madaktari bingwa, Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza, Ngusa Samike, alisema itakuwa suluhisho na ufumbuzi wa matatizo ya kiafya yanayowakabili wananchi.

"Lengo la serikali ni kufikisha huduma karibu kwa wananchi hasa wanyonge wenye kipato kidogo ikizingatiwa ni nadra kuwapata madaktari bingwa, kuanzishwa kambi hii kwa ajili ya uchunguzi wa magonjwa mbalimbali ni fursa kwa wenye matatizo ya kiafya, niwapongeze Sekou Toure kwa kubuni wazo hili na kulitekeleza," alisema.

Awali, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk. Thomas Rutachunzibwa, alisema wagonjwa wanaotoka mbali watapewa kipaumbele kupatiwa huduma hizo za kibingwa na kuwataka watu kujitokeza ili wachunguzwe afya zao.

# Wachimbaji 8 waliofukiwa kifusi waokolewa

**Na Richard Makore,** KWIMBA

WACHIMBAJI wanane kati ya tisa waliofukiwa na kifusi Novemba 8, mwaka huu katika machimbo ya dhahabu ya Mhalo yaliyopo wilayani Kwimba, mkoani Mwanza wameokolewa. Watu hao walifukiwa na kifusi hicho baada ya nguzo iliyokuwa imeshikilia udongo katika moja ya shimo walilokuwa wakichimba kukatika.

Mchimbaji mmoja, Emmanuel Issack, mpaka kufikia jana alikuwa hajaokolewa katika machimbo hayo ambapo sasa atakuwa amekaa chini ya kifusi kwa siku tisa.

Mmoja wa wachimbaji katika machimbo hayo, Musa Sitta, akizungumzia tukio hilo, alisema wenzao walifukiwa tangu Novemba 8, mwaka huu.

Alisema tangu wakati huo, wamekuwa wakihangaika kuokoa maisha yao na walianza kuwatoa kidogo kidogo na mpaka jana walikuwa wameokoa wanane wakiwa hai na kubakia mmoja.

Jana Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alifika katika machimbo hayo ili kuona hali ilivyo na kushuhudia watu wakihangaika kumtafuta kijana huyo.

Akizungumza baada ya kufika eneo la tukio, Biteko aliwataka wachimbaji hao, kuchukua tahadhari wakati wakifanya shughuli zao za uchimbaji.

Aliwataka wamiliki na wachimbaji hao kuhakikisha wanafanya kazi kwa uangalifu ili kujikinga na majanga kama hayo.

"Mjitahidi kuzingatia masuala ya usalama wa kazi ili kuepukana na majanga kama haya yaliyotokea leo," alisema Waziri Biteko.

Ajali za kufukiwa na vifusi katika machimbo ya dhahabu zimekuwa zikijitokeza katika maeneo mbalimbali yenye migodi nchini.

# DSTV YAFUNGA MWAKA KWA 'ZIGO LA SIKUKUU'

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kunogesha zaidi shamrashamra za msimu wa sikukuu, Kampuni ya MultiChoice Tanzania imetangaza ofa maalum kwa wateja wapya wa DStv yenye lengo la kuhakikisha Watanzania wengi wanapata huduma hiyo ili waweze kufurahia burudani, elimu na habari na familia zao msimu huu wa sikukuu.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo iliyopewa jina la 'ZIGO la Sikukuu, Mkuu wa Masoko wa MultiChoice Tanzania, Baraka Shelukindo, alisema kama ilivyo ada kwa DStv, kila unapofika msimu wa sikukuu hutoa ofa maalum kwa wateja wake ili kuwapa burudani.

**Shelukindo alisema wateja wa kampuni hiyo wana uhakika wa kupata huduma za aina mbalimbali katika kipindi hiki ambapo ni cha sikukuu na watu wengi wakiwamo watoto huwa likizo hivyo kuwapo kwa uhitaji mkubwa wa burudani nyumbani.**

"Kwa wale ambao bado hawajajiunga na DStv, huu ndio wakati mwafaka kwani kuna mwendelezo wa ofa maalum ya DStv Poa iliyoanza Septemba, mwaka huu, ambapo kwa kuwajali wateja wetu tuliona kuwa kuna umuhimu kwa ofa hii kuendelea kuwapo sokoni katika msimu huu wa Sikukuu. Kupitia mwendelezo wa ofa hii maalum mteja ataweza kuunganishwa kwa Sh. 59,000 na zawadi ya kifurushi kipya cha DStv Poa mwezi mmoja bila malipo. Aliongeza ofa hii inawapa uhakika wateja wetu wapya kufurahia maudhui motomoto ndani ya DStv na itadumu hadi mwanzoni Januari 2022.

Alisema sambamba na mwendelezo wa ofa hii maalum wateja wetu wa DStv pia wataendelea kupata maudhui kemkem katika ZIGO hili la sikukuu lilolosheheni burudani mbalimbali kuanzia filamu, tamthilia mpya za kinyumbani kama Danga na La Familia bila kusahau filamu za kimataifa, vipindi bora vya watoto ambao sasa wanaanza likizo ikiwamo cartoon network, Disney, Nickelodeon, CBeebies, Boomerang, JimJam na Davinci.

"Na kwa wapenzi wa michezo, msimu huu wa sikukuu watapata kufurahia mechi zaidi ya 100 ndani ya Ligi Kuu England, Laliga, Serie A, Ligi ya Mabingwa UEFA na Ligi ya Europa ndani ya DStv pekee," Shelukindo alisema.

Akifafanua zaidi kuhusu ofa hiyo maalum inayopatikana nchi nzima, Shelukindo alisema mawakala wa DStv wanapatikana kote nchini hivyo mteja atapata ofa hii na huduma ya kufungiwa DStv popote alipo kwa urahisi na haraka.

"Tunafahamu kipindi hiki cha sikukuu watu wengi husafiri kuungana na familia zao maeneo mbalimbali mijini na vijijini na kwa kulitambua hili tumejipanga kuhakikisha huduma zetu zinapatikana kirahisi kila mahali."

Amewashauri wateja wote ambao wanahitaji huduma za DStv, mbali na kwenda kwenye vituo au mawakala wa DStv, wanaweza pia kupata huduma hiyo kwa kupiga simu 0659070707 au kwa kutembelea kurasa za DStv Tanzania za mitandao ya kijamii Instagram @dstvtanzania,Twitter @DStv_Tz na Facebook @DStv(tz) huku wale wanaosafiri wanaweza kuingia katika DStv App itayowawezesha kuendelea kufurahia huduma za DStv kwenye vifaa mbalimbali kama simu janja bila gharama ya ziada. "Kwa wale wanaosafiri na wangehitaji kuendelea kuburudika na DStv, ni vyema wakatumia huduma yetu ya DStv App kwa kupakua app yetu na hivyo kuweza kutumia akaunti zao katika vifaa zaidi ya vine popote walipo nchini bila kulazimika kulipia malipo yoyote ya ziada," alisisitiza Shelukindo.




Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo (wa pili kutoka kushoto), akizungumza katika uzinduzi wa kampeni ya Zigo la Sikukuu. Kampeni hiyo ilizinduliwa rasmi jana katika Makao Makuu ya Ofisi za MultiChoice Tanzania, jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

## KMC: Tutaikaribisha Azam kwa ari mpya

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kumalizika kwa kipindi cha mapumziko ya kalenda ya FIFA, KMC imesema imejiandaa kurudi 'kivingine' katika mechi za Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara baada ya kurekebisha makosa waliyofanya kwenye michezo iliyopita.

Akizungumza na gazeti hili, Katibu Mkuu wa KMC, Walter Harrison alisema kutokana na matokeo yasiyoridhisha ambayo walipata, kikosi chake hakikuwa na mapumziko na anaamini sasa wachezaji wake wamejengeka na wako tayari kwa mapambano.

Harrison alisema mechi za kirafiki walizocheza zimemsaidia kukiimarisha kikosi cha huku benchi la ufundi likitoa mbinu mpya za ushindi.

"Matokeo ambayo tuliyapata mpaka sasa hayaakisi wachezaji tulionao na usajili ambao tumeufanya, ndiyo maana hatukuwapa mapumziko wachezaji wetu, tuliendelea na mazoezi na mechi za kirafiki.

## Dodoma yaingiwa hofu kwa Biashara

**Na Adam Fungamwango**

TAHADHARI! KOCHA Mkuu wa Dodoma Jiji, Mbwana Makata, amesema kikosi chake kimejiandaa kuivaa Biashara United kwa tahadhari kwa sababu wanaiona ni moja ya timu tishio kwenye Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara msimu huu.

Makata alisema hayo jana wakati akiendelea na maandalizi ya mechi yao itakayowakutanisha Jumapili kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, lakini akiwasifu wapinzani wao wameimarika.

"Tulianza mazoezi Jumatatu, tutacheza dhidi ya Biashara United siku ya Jumapili. Ni timu nzuri, msimu uliopita ilikuwa kwenye nafasi ya nne bora na hata kwenye mechi za kimataifa imetuwakilisha vizuri, kama si misukosuko iliyowapata, kwa hiyo inatufanya tuingie kwa tahadhari kubwa," alisema Makata.

Kocha huyo alisema anaamini timu yake inaweza kupata ushindi endapo tu nyota wake watacheza kwa ari na kwa utulivu dhidi ya wageni wao.

# *Coastal Union yaipigia hesabu Polisi Tanzania*

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Coastal Union, Melis Medo, amesema kikosi chake kipo tayari kwenda kusaka ushindi wa kwanza itakapowavaa Polisi Tanzania katika mchezo wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Chuo cha Ushirika ulioko Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Medo aliliambia gazeti hili baada ya kukosa ushindi katika michezo yao mitano iliyotangulia, wameyafanyia kazi mapungufu na sasa wachezaji wake wako fiti kwa ajili ya kupambana na hatimaye kuondoka na pointi tatu muhimu.

Kocha huyo alisema baada ya kufanyia kazi madhaifu yao, lakini amekaa na wachezaji wake ili kuwajenga kisaikolojia na kuhakikisha hawarudii makosa, lakini wakijiondoka mkiani kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Hakuna mechi rahisi kila mmoja amejiandaa vizuri, tunaenda Moshi kucheza na Polisi Tanzania, itakuwa mechi ya ushindani mkubwa kwa sababu kila mmoja anahitaji ushindi."

"Sisi tunahitaji kupata ushindi wetu wa kwanza tangu kuanza kwa msimu, wapinzani wetu wanahitaji nao matokeo mazuri, kiufundi utakuwa mchezo mzuri na kuvutia," alisema Medo.

Coastal Union ina pointi nne zilizotokana na kutoka sare mara nne na ilipoteza mchezo mmoja na kwenye msimamo wa ligi iko katika nafasi ya 12 wakati vinara ni Yanga ya jijini Dar es Salaam.

## ZISIKUPITE

### MBAPPE APEWA MUDA

REAL Madrid haitajaribu kumsajili, Kylian Mbappe, 22, ifikapo Januari badala yake itatupa ndoano kwa mshambuliaji huyo mfaransa katika dirisha lijalo la majira. ***(Mundo Deportivo)***

### COUTINHO: SIENDI NEWCASTLE

KIUNGO Mbrazil, Philippe Coutinho, 29, atawakacha Newcastle United Januari kwa sababu hana mpango wa kuondoka Barcelona. ***(Sport)***

### TRAORE SOKONI RASMI

KLABU ya Wolves iko tayari kumuuza winga wa Hispania, Adama Traore, 25, Januari wakati huu mazungumzo kuhusu mkataba mpya yakiendelea kusuasua, na klabu yake ya zamani Barcelona itachuana na Liverpool kuwania saini ya nyota huyo. ***(90min)***

### LAMPARD KUREJEA EPL

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Frank Lampard anataka kurejea katika Ligi Kuu England msimu huu akiifuatilia Leicester City iwapo Brendan Rodgers ataondoka kwenda kurithi mikoba ya Ole Gunnar Solskjaer pale Manchester United. ***(Eurosport)***

### ROONEY KUBAKIA COUNTY

WAYNE Rooney anatarajia kusalia kama kocha wa Derby County licha ya kukatwa alama tisa zaidi na kusalia shimoni kushuka daraja baada ya kuvunja sheria za fedha. ***(Sun)***

### DE BEEK ANUKIA MADRID

REAL Madrid huenda ikatupa ndoano zake kwa kiungo wa Manchester United, Donny van de Beek, 24, katika dirisha la Januari wakati huo kiungo huyo atapatikana kwa ada nafuu kutokana na kukosa nafasi ya kucheza. ***(Fichajes)***

### BARCA KUMSAJILI ADEYEMI

BARCELONA inajiandaa kuipa Red Bull Salzburg kitita cha pauni milioni 33.8 kwa ajili ya kumsajili, Karim Adeyemi, lakini Borussia Dortmund wako kwenye nafasi nzuri zaidi ya kumsajili mshambuliaji huyo Mjerumani mwenye umri wa miaka 19. ***(Sport1)***

### TARKOWSKI ABANWA

KLABU ya Burnley iko tayari nyota wake, James Tarkowski, amalizie mkataba wake msimu ujao kuliko kumuuza Januari - huku West Ham na Newcastle wakimtaka mlinzi huyo wa England. ***(Football Insider)***

### CHAMBERS KITAELEWEKA

EVERTON huenda ikatoa pauni milioni tano ili kumsajili, Calum Chambers, 26, ifikapo Januari kama watashindwa kumpata kwa mkopo mlinzi wa Arsenal, Ainsley Maitland-Niles (24). ***(Sun)***

### SMITH AMTAKA HOURIHANE

KOCHA mpya wa Norwich City, Dean Smith anapanga kuungana tena na kiungo wa Aston Villa kutoka Jamhuri ya Ireland, Conor Hourihane, 30, ifikapo Januari. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# LIONEL FURAHA TELE ARGENTINA IKIFUZU

**Kocha huyo afunguka huu ni mwaka wa aina yake kutokana na mafanikio...**

**SAO PAULO,** Brazil

KOCHA wa Argentina, Lionel Scaloni amesheherekea "mwaka wa aina yake" baada ya mabingwa hao wa Copa America kufuzu kucheza michuano ya Kombe la Dunia itakayofanyika Qatar 2022.

Licha ya kutoka sare ya bila kufungana nyumbani kwa wapinzani wao Brazil waliokwisha kufuzu, Argentina imepata nafasi ya kwenda Qatar baada ya Colombia, Uruguay na Chile kushindwa kushinda mechi zao Jumanne.

Hayo yamekuwa mafanikio makubwa kwa mwaka 2021 kwa washindi hao mara mbili wa Kombe la Dunia Argentina, ambao walimaliza miaka 28 ya kusubiri kutwaa taji la kimataifa baada ya kuifunga Brazil kwenye fainali ya Copa America Julai mwaka huu.

**"Ulikuwa mwaka wa aina yake," alisema Scaloni – ambaye alifikia rekodi ya Alejandro Sabella ya kuiongoza nchi hiyo kucheza mechi nyingi 13 bila kufungwa kwenye mbio za kufuzu Kombe la Dunia.**

"Kushinda Copa, kufuzu Kombe la Dunia bila kufungwa. Ilikuwa ni ndoto."

"Tulipata pointi nne dhidi ya timu mbili pinzani zaidi. Tulitakiwa kushinda mechi hizo. Bila shaka, tulikuwa salama zaidi.

"Kufuzu Kombe la Dunia halikuwa jambo rahisi sana kwetu, lakini ni kitu ambacho kimetuweka kwenye nafasi nzuri zaidi."

Argentina ambao wanatafuta kombe lao la kwanza la dunia tangu mwaka 1986 wapo nafasi ya pili kwenye msimamo kwa nchi za Amerika Kusini, huku zikiwa zimebakia mechi tano na ikipitwa pointi sita na vinara, Brazil na ikiipita Ecuador pointi sita ikiwa nafasi ya tatu.






# CAVANI AWATAKA MASHABIKI KUVUMILIA



**MANCHESTER,** England

EDINSON Cavani amewataka mashabiki wa Manchester United "kuwa na imani kwa timu yao" baada ya mwanzo mbaya kwa mashateni hao wekundu katika msimu huu.

United wapo nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, pointi tisa nyuma kwa vinara wa Chelsea, na imeshinda mchezo mmoja kati ya mechi sita zilizopita.

Hiyo ikiwamo kipigo cha mabao 5-0 nyumbani kutoka kwa Liverpool, ikiwa ni kipigo kikubwa zaidi tangu mwaka 1895 walipochapwa mabao 7-1 pale Anfield. Kikosi hicho cha kocha, Ole Gunnar Solskjaer Jumamosi hii kitasafiri kwenda Watford kwenye mchezo wa ligi na Cavani amewataka mashabiki kuwa na utulivu.

Akizungumza na jarida la Manchester United, nyota huyo wa kimataifa wa Uruguay amesema: "Ujumbe wangu kwa mashabiki kuwa na imani na timu yao na wachezaji ambao wanapambana kuibeba timu.

Cavani mwenye umri wa miaka 34 amefunga mabao 18 na asisti sita katika mechi 47 pale United tangu asajiliwe kwa uhamisho huru kutoka Paris-Saint Germain Oktoba, mwaka 2020.



# Van Gaal alihofia Uholanzi kutofuzu

**AMSTERDAM,** Uholanzi

LUOIS van Gaal alihofia Timu ya Taifa ya Uholanzi ingeshindwa kupata nafasi ya kufuzu kucheza fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika mwakani nchini Qatar.

Uholanzi ilipaa kileleni mwa msimamo wa Kundi G, Jumanne baada ya ushindi wa 2-0 dhidi ya Norway shukrani kwa mabao ya Steven Bergwijn na Memphis Depay.

Uholanzi sasa haijapoteza katika mechi saba tangu michuano ya Euro 2020, akishinda mara tano.

"Kwa uhakika nilikuwa na hofu baada ya kutoka sare na Montenegro, kwa uhakika nilikuwa na woga kwamba, hatutafuzu," alisema Van Gaal akiiambia NOS Journaal.

"Lakini yote kwa yote ilikuwa wiki nzuri yenye kila kitu kizuri. Tulijua kwamba, ushindi ni jambo la muhimu ili tufuzu.

"Tumefunga mabao mawili leo (juzi) na Jasper Cillessen aliendelea kucheza bila kuruhusu bao.

"Tulitawala mchezo kwa dakika 90. Norway ilitengeneza nafasi ya nyingi za kufunga."

## HABARI MICHEZO


,934,380

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 20.11.21 | 18:00 | Burnley vs Crystal Palace | 2.80 | 3.21 | 2.55 |
| 2. 20.11.21 | 18:00 | Aston Villa vs Brighton | 2.50 | 3.25 | 2.85 |
| 3. 20.11.21 | 18:00 | Newcastle vs Brentford | 2.69 | 3.24 | 2.64 |
| 4.20.11.21 | 18:00 | Wolverhampton vs West Ham | 3.01 | 3.21 | 2.41 |
| 5. 20.11.21 | 18:00 | Hull City vs Birmingham | 2.63 | 3.12 | 2.63 |
| 6. 20.11.21 | 18:00 | Reading vs Nottingham | 2.89 | 3.18 | 2.39 |
| 7. 20.11.21 | 20:00 | Lazio vs Juventus | 2.78 | 3.36 | 2.48 |
| 8. 20.11.21 | 20:45 | Sparta Rotterdam vs Twente | 2.61 | 3.20 | 2.61 |
| 9. 20.11.21 | 22:45 | Fiorentina vs AC Milan | 3.09 | 3.39 | 2.26 |
| 10. 21.11.21 | 15:00 | Brest vs Lens | 3.03 | 3.43 | 2.26 |
| 11. 21.11.21 | 17:00 | Salernitana vs Sampdoria | 3.00 | 3.29 | 2.37 |
| 12. 21.11.21 | 17:00 | Troyes vs St Etienne | 2.35 | 3.34 | 2.94 |
| 13. 21.11.21 | 17:00 | Metz vs Bordeaux | 2.42 | 3.28 | 2.88 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 18 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 10:30 | 2527 | Henan Jianye W vs Beijing Baxy W | 2.99 | 3.66 | 2.03 |
| 13:00 | 1520 | FC Noravank vs Ararat Yerevan | 6.00 | 3.87 | 1.48 |
| 14:00 | 1144 | Leixoes SC U23 vs FC Famalicao U23 | 2.47 | 3.29 | 2.56 |
| 14:15 | 1498 | Pusamania Borneo vs Persipura Jayapura | 1.69 | 3.67 | 4.25 |
| 14:30 | 3244 | Padideh Mashhad vs Zob Ahan | 3.95 | 2.89 | 2.00 |
| 15:00 | 1377 | Indjija vs Red Star Belgrade | 16.35 | 7.89 | 1.10 |
| 15:00 | 3986 | FK Zeleznicar Pancevo vs FK Graficar Beograd | 1.38 | 4.23 | 7.31 |
| 15:45 | 1812 | Rampla Juniors vs Defensor Sporting | 4.15 | 3.52 | 1.74 |
| 16:00 | 1490 | Africain vs Sportive Zarzis | 2.35 | 2.96 | 2.97 |
| 16:00 | 2487 | Gorilla FC vs AS Kigali | 9.69 | 5.43 | 1.23 |
| 16:00 | 2685 | US Ben Guerdane vs ES Hammam Sousse | 1.66 | 3.37 | 5.01 |
| 16:00 | 2995 | Farco FC vs Misr Lel Makasa | 2.12 | 3.15 | 3.49 |
| 16:00 | 3439 | ES Metlaoui vs Club S Hammam-Lif | 1.74 | 3.14 | 4.83 |
| 16:00 | 4218 | AS Slimane vs CS Chebba | 2.09 | 2.93 | 3.55 |
| 16:00 | 4695 | Espoir FC vs Gicumbi | 1.54 | 4.10 | 6.00 |
| 16:30 | 3348 | PSM Makassar vs PSS Sleman | 2.01 | 3.47 | 3.18 |
| 17:00 | 4799 | Novi Pazar vs Cukaricki St | 5.02 | 3.77 | 1.57 |
| 17:30 | 4251 | Sanat Naft Abadan vs Gol Gohar | 3.80 | 2.84 | 2.06 |
| 18:00 | 1184 | US Monastir vs Olympique de Beja | 1.79 | 3.11 | 4.55 |
| 18:00 | 1671 | Leon U20 vs Santos Laguna U20 | 2.31 | 3.23 | 2.80 |
| 18:00 | 1775 | Rio Ave U23 vs FC Vizela U23 | 2.09 | 3.43 | 3.04 |
| 18:30 | 5216 | Eastern Company SC vs Coca Cola | 3.30 | 2.85 | 2.37 |
| 20:45 | 5765 | Wolfsburg W vs Juventus Women | 1.30 | 5.19 | 7.31 |
| 21:00 | 1962 | Bourg Peronnas vs Chambly | 1.62 | 3.67 | 5.09 |
| 21:00 | 2145 | El Ittihad Alexandria vs El Gouna | 2.11 | 3.25 | 3.40 |
| 21:00 | 4158 | Ceramica Cleopatra vs National Bank | 2.43 | 3.07 | 2.97 |
| 21:30 | 3640 | Petrolul Ploiesti vs Concordia Chiajna | 2.02 | 3.17 | 3.46 |
| 22:30 | 1881 | Albion FC vs Rocha FC | 1.39 | 4.22 | 6.91 |
| 23:00 | 2585 | Union Santa Fe vs Defensa Justicia | 2.41 | 3.04 | 2.80 |
| 23:00 | 3046 | Centro Espanol vs Juventud Unida SM | 2.64 | 2.93 | 2.64 |
| 23:00 | 3627 | Real Madrid W vs Paris Saint Germain W | 6.36 | 4.72 | 1.37 |
| 23:15 | 5870 | Sporting Lisbon vs Varzim | 1.08 | 8.07 | 21.15 |

### IJUMAA - 19 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 1742 | Club Cortulua vs Leones FC | 2.19 | 3.18 | 3.04 |
| 00:30 | 5043 | Once Municipal vs Isidro Metapan | 1.64 | 3.56 | 4.81 |
| 01:00 | 2862 | Universidad Catolica vs Nublense | 1.63 | 3.71 | 4.62 |
| 01:00 | 4036 | Uruguay Montevideo FC vs Central Espanol FC | 2.41 | 3.04 | 2.80 |
| 01:15 | 3819 | Patronato Parana vs Lanus | 2.89 | 3.17 | 2.28 |
| 02:00 | 2223 | Unan Managua vs Deportivo Ocotal | 2.29 | 3.19 | 2.85 |
| 02:00 | 2951 | Tepatitlan FC vs Leones Negros Udg | 2.15 | 3.17 | 3.12 |
| 02:00 | 4290 | Real Cartagena vs Chico | 3.09 | 2.94 | 2.29 |
| 03:00 | 1236 | Sampaio MA vs Cruzeiro | 3.03 | 2.84 | 2.39 |
| 03:00 | 2570 | ART Municipal Jalapa vs Juventus Managua | 2.51 | 3.23 | 2.55 |
| 03:00 | 3555 | Sport Recife vs Bahia BA | 2.45 | 2.94 | 2.84 |
| 03:30 | 5784 | Banfield vs Aldosivi | 1.56 | 3.67 | 5.41 |
| 03:45 | 1979 | Nacional (URU) vs CS Cerrito | 1.36 | 4.61 | 6.72 |
| 04:00 | 4148 | Fortaleza (COL) vs Llaneros FC | 2.09 | 3.26 | 3.17 |
| 05:00 | 4625 | Deportivo Walter Ferreti vs Real Esteli | 3.04 | 3.19 | 2.18 |
| 10:30 | 2025 | Changchun Huaxin W vs Wuhan Jiangda W | 3.04 | 3.47 | 2.07 |
| 11:45 | 1217 | Melbourne City vs Brisbane Roar | 1.49 | 4.53 | 5.51 |
| 13:30 | 2156 | Gasogi United vs Rutsiro FC | 1.78 | 3.38 | 4.15 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MADRID KUTOMSAJILI MBAPPE JANUARI




**PARIS,** Ufaransa

REAL Madrid haitamfuatilia nyota wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe wakati wa dirisha la Januari, limedai gazeti la Mundo Deportivo.

Miamba hao wa Hispania wamekuwa wakihusishwa na mpango wa kumsajili nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa kwa muda mrefu.

Mbappe ameonyesha nia ya kutaka kuondoka Paris Saint-Germain kwa siku za usoni hapo.

Los Blancos imekuwa ikihaha kumshawishi nyota huyo mwenye umri wa miaka 22, huku mkataba wake unafikia ukingoni mwishoni mwa msimu huu.

Kumekuwa na uvumi kuhusu majaliwa ya Mbappe, ambaye amekataa kuongeza mkataba mpya na klabu hiyo kwa madai anataka kuondoka.




# *Deschamps awasifia Benzema, Mbappe*

**PARIS,** Ufaransa

DIDIER Deschamps amesifia 'upatina' kati ya Karim Benzema na Kylian Mbappe baada ya Ufaransa kumaliza kampeni ya kufuzu kucheza Kombe la Dunia kwa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Finland.

Ushindi huo ulizima ndoto za Finland kwenda kucheza hatua ya mtoano wakati Ukraine ikimaliza nafasi ya pili katika Kundi D.

Ufaransa ilifuzu kwenda Kombe la Dunia bila kufunga katika mechi 27 zilizopita kwenye michuano yote, ingawa walikuwa na wakati mbaya kwenye michuano ya Euro 2020 kwa kufungwa na Uswisi hatua ya 16.

"Hatutakiwi kumsahau Antoine Griezmann," alisema Deschamps baada ya kuulizwa kuhusu Benzema na Mbappe.

"Ilionekana rahisi kwa sababu ya wachezaji wawili kuwa na ubunifu na wanacheza kwa uelewano mzuri zaidi.

"Upatina wao kwenye michuano ya kufuzu Kombe la Dunia ulikuwa mzuri zaidi na ndio umechangia timu kuwa kwenye ubora wa hali ya juu.

# Michezo

Alhamisi Novemba 18, 2021

**Nipashe**




Lionel furaha tele Argentina ikifuzu UKURASA 21



Beki wa kati wa Simba, Erasto Nyoni (kulia), akijaribu kumiliki mpira kwenye mazoezi ya timu hiyo jana kabla ya kuelekea Mwanza kuwakabili Ruvu Shooting katika mchezo wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara utakaochezwa kesho Ijumaa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza. **PICHA: SIMBA SC**

## Ruvu yaitisha Simba

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, Simba, wamefika salama Mwanza huku wapinzani wao, Ruvu Shooting wakitamba wako kamili kuhakikisha wanaibuka na ushindi katika mchezo huo utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini humo.

Kocha Msaidizi wa Simba, Thierry Hitimana, aliliambia gazeti hili wamefika Mwanza na leo watakamilisha programu ya mwisho ya mazoezi kwa ajili ya kuwakabili wapinzani wao, Ruvu Shooting.

"Tumejipanga na tunaamini tutarudi kwenye ubora wetu, tumeyafanyia kazi mapungufu mbalimbali tuliyoyabaini kwenye timu yetu kwa ushirikiano na kocha mpya (Pablo Franco), tunaamini tutakuwa na kiwango kizuri," Hitimana alisema.

Aliongeza wachezaji wao waliokuwa majeruhi ambao walikosa mechi mbili zilizopita akiwamo Ousmane Sakho hali zao zimeimarika na uamuzi wa kucheza umebakia chini ya Pablo ambaye kesho ataiongoza Simba kwa mara ya kwanza kwenye mchezo wa ligi.

Ofisa Habari wa Ruvu Shooting, Masau Bwire, alisema jana wachezaji wao wako tayari kwa mchezo huo wa raundi ya sita ambao unatarajiwa kuwa na ushindani kutoka kila upande.

Bwire alisema wachezaji wao wote wako fiti na wana ari ya kuendeleza rekodi nzuri dhidi ya mabingwa hao watetezi wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16.

"Tumeshajiandaa vizuri kuwapapasa Simba, tuko tayari kwa mchezo huo, hatuna hofu na hilo wapinzani wetu wanalifahamu, tunawaambia sisi ndio wataalamu wa mpira hapa nchini," Bwire alisema.

Simba imecheza mechi tano na imevuna pointi 11, ikishinda mechi tatu dhidi ya Dodoma Jiji, Polisi Tanzania na Namungo FC huku ikitoka sare na Biashara United na Coastal Union.

# Yanga, Namungo mtafutano

**Na Saada Akida**

### Nabi aweka wazi wataikabili Namungo kivingine kwa sababu...

WAKATI kikosi cha Yanga kikiwasili salama mkoani Lindi kwa ajili ya kuivaa Namungo FC, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Nesreddine Nabi, amesema kutakuwa na mabadiliko ya kimbinu kuelekea katika mchezo huo wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Ilulu.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema wamefanya maandalizi ya kutosha na wamebadili mbinu kwa ajili ya kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mchezo huo na kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi hiyo.**

Nabi alisema wanawafahamu vyema wapinzani wao na anaamini wataongeza umakini lakini wakiwaheshimu wenyeji wao ambao watakuwa wanacheza kwenye uwanja wa nyumbani.

Alisema mechi mbili za kirafiki walizocheza huko Visiwani Zanzibar zilikuwa na malengo maalum ya kutengeneza mifumo na mbinu mpya ambazo anatarajia kuzitumia katika michezo iliyopo mbele yao hasa na itakuwa inabadilika kulingana na aina ya timu watakayokutana nayo.

"Kipindi cha mapumziko ya kalenda ya Fifa kulikuwa na kazi pia ya kutafuta mifumo mipya ambayo tutaitumia kuanzia sasa, na hasa baada ya kuumia kwa Yacouba Sogne ambaye alikuwa katika mipango ya kikosi cha kwanza,".

"Kumkosa nyota huyo (Sogne), tunalazimika tuwe na mbadala wake ambaye anaweza kuwa Mukoko Tonombe au Farid Mussa, hii inatokana na kila mmoja anaweza kufanya mabadiliko kuendana na mbinu ambazo tutazitumia ili kukabiliana na mpinzani wetu," alisema Nabi.

Kocha huyo alisema kulingana na nyota hao kufanya vizuri katika mechi za kirafiki, ana imani watafanya anachokitarajia katika mechi za ligi zinazofuata licha ya kutoweka wazi mbinu ambazo wataingia nazo katika mchezo wao dhidi ya Namungo.

Aliongeza ligi ya msimu huu imekuwa na ushindani mkubwa na hiyo imetokana na kila timu kufanya maandalizi mazuri na kujiimarisha tofauti na zilivyokuwa katika misimu iliyopita.

Alisema kila mechi kwao ni sawa na fainali na wataingia uwanjani kwa lengo moja la kupata pointi tatu muhimu na si vinginevyo.

"Tumeshinda mechi zote tano, ila hatupaswi kuona tuko bora zaidi ya wapinzani wetu, tunahitaji kuwa makini na kila mchezaji anayepata nafasi ya kucheza anatakiwa kujitoa kwa ajili ya kupata matokeo chanya ambayo yatatupeleka kufikia malengo yetu," kocha huyo alisema.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli aliliambia gazeti hili wachezaji wao wapo tayari kwa mchezo huo na wanatarajia kuendelea kuwapa furaha wanachama na mashabiki wao.

"Kama ambavyo tumemaliza mechi zetu tano ambazo zimepita kwa ushindi, ndivyo ambavyo tunataka iwe hivyo kwa mechi zetu ambazo zinafuata ikiwa ni pamoja na hii dhidi ya Namungo," alisema Bumbuli.

Yanga itashuka dimbani kuwakabili Namungo wakiwa na kumbukumbu ya kutoa kichapo cha mabao 3-1 kwa Ruvu Shooting, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.

Mabao ya Yanga katika mchezo huo yalifungwa na Feisal Salum, Djuma Shabani na Mukoko huku lile la Ruvu Shooting lilipachikwa wavuni na Shabani Msala.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >